

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TAZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 21 Julai, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 247

**Mkoa wa Shinyanga Kuwa na Hospitali ya Mkoa Inayostahili**

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga hauna hospitali ya Mkoa yenyе viwango kiasi kwamba ile iliyopo ni sawa na kituo cha afya kikubwa na kwa kuwa Mkoa wa Shinyanga ni wa kwanza kwa idadi ya watu nchini:-

- (a) Je, ni lini Mkoa huu utakuwa na hospitali ya Mkoa yenyе viwango stahili?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani katika kusaidia Manispaa ya Shinyanga kuwa na hospitali yake?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. AGGREY D. J. MWANRI K.N.Y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Dokta Charles Mlingwa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hospitali ya Mkoa Shinyanga ilijengwa kwa mara ya kwanza mwaka 1947 kikiwa ni kituo kidogo cha kutolea huduma za afya. Kituo hicho kiliendelea kukua hadi mwaka 1974 kituo hicho kilipobadilishwa kuwa hospitali ya mkoa baada ya kuongezewa baadhi ya majengo muhimu. Pamoja na jitihada za kuongeza majengo na mahitaji mengine muhimu kama vile watumishi na vifaa, hospitali hiyo kwa sasa bado haijatimiza vigezo vya kuwa hospitali kamili ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni azma ya Serikali kuhakikisha kila Mkoa, ukiwemo Mkoa wa Shinyanga, unakuwa na hospitali yake ya Mkoa yenye viwango vinavyokubalika. Aidha, ni uamuvi wa Serikali kuwa hospitali za Mkoa zitapandishwa hadi kuwa Hospitali za Rufaa za mkoa husika. Katika kutekeleza azma hiyo, Serikali imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya upanuzi na ukarabati wa majengo sambamba na kufundisha na kupeleka wataalam ambao ni mabingwa. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Serikali ilitenga shilingi milioni 520 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa majengo ya hospitali ya Mkoa wa Shinyanga. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2008/2009, Serikali imetenga shilingi milioni 600 kwa kuendeleza ukarabati na upanuzi wa hospitali hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga, namshauri Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga ili wakiona inafaa, basi waweke mradi wa ujenzi wa hospitali ya Manispaa kwenye mipango yao ya maendeleo. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itakuwa tayari kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu ujenzi wa hospitali hiyo pale itakapohitajika.

**MHE. DR. CHARLES O. MLINGWA:** Kwa kuwa sera za Chama cha Mapinduzi zinakwenda sambamba na azma ya kuwa na huduma bora za afya nchini:-

(i) Wizara inajishughulisha vipi kuona kuwa Manispaa ya Shinyanga, inakuwa na Hospitali yake ili kusudi ijiridhishe kuwa sera za afya zinatimizwa ipasavyo?

(ii) Ningependa kujua Wizara inajishughulisha vipi kuona kuwa, na ninashukuru kwamba leo Serikali imesema kuwa haijatimiza vigezo vya kuwa Hospitali ya Mkoa, hospitali ya Mkoa inajengwa sehemu ambayo itakuwa na nafasi ya kutosha kuweza kujenga hospitali ya mkoa wa Shinyanga.

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. AGGREY D. J. MWANRI K. N. Y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa

Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba suala la sera ni suala ambalo linahusu Wizara, wala sio suala la kusema kwamba ni Manispaa yenyewe au nini.

Hili ni suala la Wizara yenyewe. Ndio maana katika majibu ambayo tumeyatoa hapa tumesema popote patakapohitajika ushauri wa aina yoyote ikiwa ni pamoja na *ku-formulate* hizo sera sisi kama Wizara tuna hakika kwamba tutafanya hivyo na mimi nitahakikisha kwamba namfikishia Mheshimiwa Waziri wa Afya, rai hiyo, kwa sababu ni wajibu wake wa msingi huo.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo limeulizwa hapa linahusu sasa habari ya kufikiri mahali pengine ambapo panafaa kuweka hospitali ya mkoa.

Kama Mheshimiwa Mbunge, alivyozungumza kwa kweli pale palikuwa ni kituo cha afya tu, kikapandishwa kikafikishwa hapo. Unapokuwa na hospitali ya mkoa, viko vigezo ambavyo vinakufanya uitwe Hospitali ya Mkoa, ni pamoja na wataalamu, ni pamoja na kuwa na *X-Ray* ambayo ni *heavy duty*, ni pamoja na kuwa na *wards* za kutosha na eneo hili linalozungumzwa, mimi mwenyewe nimewahi kufika pale pamoja na kwamba najibu kwa niaba ya Wizara ya Afya, ni eneo dogo.

Kwa hiyo, ni suala sasa la wadau wote muhimu. Hili haliwezi kuwa ni la mtu mmoja na wala la Serikali, litakuwa ni Mkoa wa Shinyanga wenyewe pamoja na Manispaa na wale wengine wote wanaohusika kufika mahali wakaamua kwamba wao wanafikiri kwamba hospitali ya mkoa ihamie wapi kwa maana hii anayozungumzia Mheshimiwa Mbunge, lakini Wizara itakuwa tayari kutoa ushirikiano.

Na. 248

### **Mifuko ya *Import Support***

**MHE. CHARLER N. KEENJA** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya 80 na 90 uchumi wa nchi yetu ulikuwa mbaya sana, ambapo ulianzishwa Mfuko Maalum ulijulikana kama *Import Support Fund*.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kilitengwa kwa kipindi chote mfuko huo ulipokuwepo na ni kiasi gani kilikopeshwa?

(b) Je, ni watu na makampuni mangapi yalifaidika na mikopo hiyo na ni kiasi gani cha mikopo kimerejeshwa?

(c) Je, matatizo ya wakopaji kutorejesha fedha za mfuko yanatofautianaje na yale ya *EPA*?

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Ubungo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya *Commodity Import Support, CIS*, ni 222,920,286,957/= tarehe 30 Juni, 2003 na hadi sasa kiasi chote kimekopeshwa kwa watu, makampuni binafsi na taasisi mbalimbali za umma.

(b) Mheshimiwa Spika, kufikia Septemba, 2007, watu binafsi, makampuni binafsi na taasisi za umma zipatazo 980 zilikuwa zimenufaika na mikopo hii ya *Commodity Import Support*. Kiasi kilichorejeshwa ni Sh. 119,221,222,212/=.

(c) Mheshimiwa Spika, matatizo ya urejeshwaji wa fedha za mpango wa *Commodity Import Support* hayafanani na masuala ya *EPA* kwa sababu *Commodity Import Support* ni mikopo iliyotolewa kwa waliopewa baada ya kukamilisha masharti na vigezo vilivyowekwa.

Hazina ilitoa matangazo katika magazeti kukaribisha maombi na mwombaji, alitakiwa kuomba mkopo kulingana na sekta zilizokuwa zimepewa kipaumbele kama zilivyoordheshwa kwenye matangazo hayo. Kwa mfano kilimo, viwanda, biashara, madini, usafirishaji, ujenzi na nishati.

Mheshimiwa Spika, vigezo vilivyowekwa ni pamoja na Mwombaji kuwa na hati ya Usajili wa Kampuni au biashara, pamoja na namba ya utambulisho ya kodi, uthibitisho wa benki kuhusu uwezo wa mkopaji kutumia fedha za mkopo kwa lengo alilolitaja na iwapo mkopaji hadaiwi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kabla mkopaji hajaruhusiwa kutumia mkopo, ultakiwa kulipia asilimia 30 ya mkopo alioomba kama malipo ya awali. Baada ya kulipia asilimia 30, alitakiwa kuingia katika Mkataba wa Deni na Hazina ambapo alitakiwa kuwasilisha mtiririko wa marejesho ya asilimia 70 ya deni lililobaki katika muda wa malipo usiozidi miezi 18.

**MHE. CHARLES N. KEENJA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili, madogo sana, ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kwanza kiasi cha fedha ambacho kimesharejeshwa ni zaidi kidogo ya nusu ya pesa zilizokopeshwa. Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba kiasi kilichobakia kinarejeshwa mapema iwezekanavyo na zikirejeshwa zitatumikaje?

Mheshimiwa Spika, swal la pili, Wizara ndiyo iliyokopesha pesa hizi, lakini baadaye wamehamisha uzimamizi wa mikopo hii kwenda benki ya rasilimali. Ni sababu gani zilizosababisha kuhamishwa kwa wajibu huo na kumekuwa na mafanikio gani? Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI:**  
Mheshimiwa Spika, hatua za ziada ambazo zinachukuliwa sasa, kwa kweli ni mbili kuu. Ya kwanza ni kwamba, tumekuwa wakali kidogo na tumeongeza nguvu katika kutaka kukusanya haya madeni. Ni madeni ambayo yalitokana na nia nzuri ya Serikali ya kuendesha viwanda vyetu na biashara nchini na tunadhani kwamba wakati umefika sasa na muda umepita wa hao wenzetu kulipa madeni haya. Lakini nataka kusema kwamba matatizo tuliyonayo hapa ni kwamba wakati wale wenzetu walipewa hizi pesa katika fedha za kigeni na walitakiwa warejeshe kwa kiwango cha thamani ya fedha zile ya wakati ule anaporesha sasa wanajikuta kwamba inabidi warejeshe fedha nyingi zaidi kwa Tanzania, kuliko zile walizokopa. Lakini hilo ndilo lililokuwa kwenye mkataba na tunadhani kwamba inabidi waheshimu.

Mheshimiwa Spika, lakini hatua ya pili ambayo tunaichukua ni kumtafuta mkusanya madeni na huyo kashapatikana na nia yetu na lengo letu hapa ni kwamba sio tu akusanye yale madeni lakini kutokana na ile mikataba waliyoingia na Serikali na Hazina, walitoa dhamana na kwa hiyo huyu atakayepewa hii kazi ya kukusanya haya madeni tutategemea kwamba pale ambapo halipwi, basi anashika ile dhamana na kuiweka kwenye mnada ili fedha za Serikali zirudi.

Mheshimiwa Spika, swal la pili la Mheshimiwa Keenja, kwamba haya madeni yalihamishiwa *TIB*. Wakati wa kurejesha waliokuwa wanakusanya haya madeni ni *TRA* chini ya sheria ya *Commodity Import Support Regulation Act* ya 1992 pamoja na Hazina yenye. *TRA* bado inaendelea kukusanya madeni haya na ile sehemu ambayo ingekusanya na Hazina, imehamishiwa *TIB* ili kuongeza hiyo kasi na juhudzi za kukusanya haya madeni ambazo nimetaja. (*Makofî*)

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swal la nyongeza. Kwa sababu mikopo hii ilikuwa imelenga maeneo mahsusii katika maeneo maalum ikiwemo kilimo, na masharti ilikuwa ni baada ya miezi 18, sasa Serikali ilikuwa wapi baada ya miezi 18 kudai marejesho hayo na imekurupuka sasa wakati limeibuka hili suala la *EPA*?

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI:**  
Mheshimiwa Spika, kwanza nimkatalie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali haijakurupuka na Serikali haikurupuki. Lakini la pili tunesikia Mheshimiwa Keenja kasema na takwimu nilizotaja hapa ndivyo zinavyodhihirisha kwamba tumekusanya zaidi ya shilingi bilioni 119 kati ya shilingi bilioni 222. Lakini la pili katika madeni huwezi kutegemea kwamba wale ambao wanakopa watakulipa ndani ya muda ule ule ambao mmekubaliana na kwa sababu mbalimbali ambazo wala sina haja ya kuingia katika undani wake.

Tulipeana miezi 18, tuliambizana kwamba kama usipolipa ndani ya miezi hii 18 utaanza kulipa kwa adhabu ya riba ambayo ni sawasawa na riba ambayo Benki Kuu inatoza Serikali au mabenki ya biashara wakikopa na vilevile utalipa kwa *exchange rate* ya wakati ule, tunadhani hiyo ni adhabu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema sasa hivi, tunaongeza juhudni tunataka fedha hizi zirudi ziingie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ili ziwe sehemu ya mapato ya Serikali ili ziweze kuingia kwenye mgawanyo na matumizi ya Serikali. (*Makofi*)

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Kwanza naipongeza Serikali, imejitahidi.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa Aprili, Serikali ilitoa *last warning* ya miezi mitatu kwa hawa waliokopeshwa na miezi mitatu hiyo imekwisha na Mheshimiwa Waziri, anasema wamekuwa wakali. Sidhani kama wamekuwa wakali. Je, baada ya hii miezi mitatu kwisha ukali mliouongeza ni upi? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI:** Mheshimiwa Spika, ukali tuliosema sio kupiga hawa Waheshimiwa rungu vichwani. Ulikuwa ni ukali wa kuwahamasisha walipe na warejee kwenye ile mikataba yao ambayo waliingia na Serikali. Kwamba baada ya miezi 18 wangeliwa riba ambayo sio haba na vilevile kwa sababu ya mporomoko wa shilingi yetu, gharama ya wao kulipa ingekuwa kubwa zaidi. Lakini vilevile kwa sasa hivi kama nilivyosema, ni kweli tumekuwa wakali kidogo na tumeona mafanikio yake.

Pamoja na kuchukua hatua za kuhamishia ile juhudni kutoka Hazina kwenyewe kupeleka *TIB* na kukaa na wenzetu wa *TRA* na kuhamasishana kukusanya fedha za Serikali na vilevile huyu jamaa tuliyesema atapewa kazi ya kukusanya haya madeni tumemwomba atumie ule mkataba. Walitoa dhamana, kama watashindwa kulipa, basi ile dhamana ifidie lile deni. Huo ndio ukali wa Serikali. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nashukuru Naibu Waziri, umetafsiri vizuri ukali. Maana yake sio masuala ya kuvunja tena sheria au kuwapiga watu. Tunaendelea Waheshimiwa. Bado tuko kwenye Wizara hiyo hiyo. Swali linalizwa na Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini.

Na. 249

### **Utendaji wa Kamati ya Sera ya Fedha**

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA** aliuliza:

Kwa kuwa, Kamati ya Sera za Fedha (*Monetary Policy Committee*), ni muhimu sana katika kusimamia utekelezaji wa Sera za Fedha hapa nchini:-

- (a) Je, Kamati hiyo imefanya vikao vingapi kwa mwaka?
- (b) Je, Kamati imetumia utaratibu gani wa kutoa taarifa za mambo muhimu yanayojadiliwa na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali na Benki Kuu katika kukabiliana na changamoto za kiuchumi hasa kwenye maeneo ya ujazi wa fedha na mwenendo wa mifumo ya riba katika uchumi wetu?

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, Mbunge wa Tabora Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu, kifungu 12(6) kinaeleza kwamba Kamati ya Sera ya Fedha itakutana mara kwa mara katika kutekeleza majukumu yake. Kiutendaji Kamati ya Sera ya Fedha hukutana kila mwezi. Kutokana na utaratibu wa kukutana mara moja kwa mwezi, idadi ya vikao vya Kamati hii kwa mwaka ni kumi na mbili. Hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2007/2008, Kamati hii ilikuwa imefanya vikao 123 toka kuundwa kwake.

(b) Mheshimiwa Spika, katika siku za nyuma, Kamati ya Sera ya Fedha haikuwa na utaratibu wa kutoa taarifa ya mambo yanayojadiliwa katika vikao vyake. Hata hivyo, Kamati imeanzisha utaratibu unaomwezesha Mwenyekiti wake ambaye ni Gavana wa Benki Kuu, kufanya mikutano na Watendaji Wakuu wa mabenki nchini kila baada ya Mkutano wa Kamati ya Sera ya Fedha, kuelezea maamuzi ya Kamati kuhusu muelekeo na malengo ya Sera ya Fedha na pia mwelekeo wa viashiria mbalimbali vya maendeleo ya uchumi nchini.

Mkutano wa kwanza wa aina hii ulifanyika tarehe 08 Januari, 2008. Vilevile, Gavana wa Benki Kuu ameanzisha utaratibu wa kukutana na waandishi wa habari mara moja kwa kila kipindi cha robo mwaka. Mkutano wa kwanza kati ya Gavana na waandishi wa habari ulifanyika tarehe 14 Machi, 2008.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa za kina kuhusu mwenendo wa uchumi na viashiria vyake hutolewa kwa njia ya ripoti mbalimbali zinazochapiswa na Benki Kuu na kusambazwa kwa wadau. Kwa mfano, taarifa ya Mapitio ya Uchumi ya Mwezi, *Monthly Economic Review*, chapisho la takwimu za uchumi, *Quarterly Economic Review* na taarifa ya mwaka, *Annual Economic and Operations Report*, ambayo hutolewa kila mwisho wa mwaka wa fedha.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa ruhusa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Naibu Waziri, kwa majibu yake. Swali langu la kwanza ni kuhusu riba baina ya amana na mikopo. Pengo baina ya riba hizi mbili ni kubwa sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, atuambie Benki Kuu inaishauri nini Serikali katika kupunguza pengo hili baina ya amana na mikopo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili ni kwamba, bei ya petroli inapangwa na soko la dunia, sisi hapa nyumbani katika bei hiyo tunaongeza kodi. Je, Benki Kuu kama msimamizi mkubwa wa shughuli za kiuchumi hapa nchini, kodi iliyoko kwenye mafuta inaongeza bei ya mafuta na kwa hiyo kuathiri bei zote za bidhaa mbalimbali hapa nchini; Benki Kuu inaishauri nini Serikali, juu ya tatizo hili? (*Makofit*)

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI:**  
Mheshimiwa Spika, swali la kwanza kuhusu riba, ushauri wa Benki Kuu kwa Serikali. Kwanza tukumbuke kwamba Benki Kuu na Serikali wanasmamia sera mbili ambazo lazima zishabihiane.

Benki Kuu inasimamia *Monetary Policy*, yaani Sera ya Fedha na Serikali inasimamia *Fiscal Policy*, Sera ya Fedha Matumizi ya Serikali na Kodi. Kila mmoja kati ya sisi wawili, Serikali na Benki Kuu, tuna sehemu ya kufanya katika kudhibiti riba. Tofauti kati ya riba ambayo Benki za Biashara zinakopesha na ambazo zinakopa kwa maana ya zile amana ambazo zinawekwa kwenye benki. Upande wa *Monitory Policy*, tunajua kwamba Benki Kuu kwa mfano, imedhamiria kwamba haitauza hati fungani ama *treasury bills* isipokuwa kwa kulipa zile ambazo zinaiva.

Lakini kwa upande wa Serikali vilevile, kwenye *Fiscal Policy*, kwenye Sera ya Matumizi ya Serikali na Kodi, Serikali imesema kwamba haitakopa kutoka kwenye uchumi kuititia kwenye njia hizo ili zile riba ambazi zinatokana na uuzaaji wa zile hati fungani pamoja na *treasury bills* zishuke.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tunajua kwamba Benki za Biashara, ile riba wanayotoza kwenye mikopo inatokana na ile *discount rate* na kile kiwango cha riba ambacho Benki Kuu, inakokotoa kutokana na wastani wa kipimo cha *treasury bill*, basi ni dhahiri kwamba kama kile kiwango cha *treasury bill* cha Benki Kuu kiko chini, basi na kiwango cha riba kwa upande wa *Commercial Banks* kitakuwa chini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei ya mafuta, ni kweli hatuna uwezo wa kuzuia mfumko wa bei ya mafuta duniani, lakini kwenye *consumer price index* yetu sio mafuta ndio yanayosukuma kile kiwango cha mfumko wa bei, ni chakula ambacho 55.90% ndio inayokupa kwa mfano 7% ama 9.2% tunayozungumzia sasa hivi. Lakini ni kweli kwamba mafuta ambayo ni 9% katika ukokotoaji wa ile *price index* una *impact* sana kwenye mfumko wa bei na kwa hiyo naweza kukubaliana na wewe kwamba ndiyo, mafuta na yenye yanachangia kwenye kukua kwa *inflation*. Ee bwana, nimekujibu. (*Makofit/Kicheko*)

**SPIKA:** Naona ilikuwa ni mapambano baina ya wachumi. Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Sanya, swali la nyongeza. (*Makofit/Kicheko*)

**MHE. IBRAHIM M. SANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina swalii moja dogo la nyongeza. Je, Serikali inachukua hatua gani katika kudhibiti mporomoko wa thamani ya Shilingi?

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA UCHUMI – MHE. JEREMIA S. SUMARI:** Mheshimiwa Spika, nitatoa hatua moja tu ambayo ni ya hivi karibuni, kwamba Benki Kuu, ambayo ndio msimamizi mkuu chini ya sera hiyo niliyosema ya fedha imekuwa ikiuza sana fedha za kigeni kwenye soko na matokeo yake ni kwamba kumekuwa na fedha nyingi za kigeni kwenye soko na matokeo yake ni kwamba shilingi yetu imepanda thamani. Lakini kama tunavyojua, tumeshasikia malalamiko tayari kwamba kwa kufanya hivyo wakulima wetu na wenyewe wameathirika kidogo, lakini hilo ni suala lingine.

Na. 250

#### **Hitaji la Vyoo katika Barabara Kuu Nchini**

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wakandarasi wanapo jenga barabara kuu hapa nchini hawaelekezwi kujenga vyoo katika vituo maalum; na kwa kuwa, wasafirishaji wengi hasa wenyewe mabasi wana tabia ya kuwashusha wasafiri kujisaidia hovyo barabarani bila ya kujali madhara yake:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kubadilika na kuwataka wakandarasi kujenga vyoo katika baadhi ya vituo katika barabara kuu zote nchini?

(b) Je, Serikali ina taarifa kuwa wenyewe mabasi hufanya tabia hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Miundombinu, inatambua umuhimu wa ujenzi wa vyoo katika barabara kuu nchini ili kulinda heshima na usalama wa wasafiri na kuzuia uharibifu wa mazingira.

Serikali imeanza kulifanyia kazi suala hili kwa kuweka mikakati ya makusudi ya ujenzi wa vyoo na maegesho ya magari katika baadhi ya vituo vya barabara kuu nchini. Tayari kwenye barabara ya Makuyuni – Ngorongoro kumejengwa vyoo vitatu kwenye maegesho ya magari ambavyo vinatumika ipasavyo. Tutaendelea kutambua barabara mbalimbali ambapo huduma hii itahitajika hasa zile zenye usafiri wa masafa marefu.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara kuitia wakala wa barabara nchini, *TANROADS*, itazingatia marekebisho katika mikataba mipy ya usanifu wa ujenzi wa barabara kwa kuongeza kipengele kinachowataka wataalamu, washauri na wakandarasi watakaojenga barabara kuu kuainisha maeneo yatakayofaa kwa ujenzi wa maegesho ya magari na vyoo.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninapenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake mazuri. Hata hivyo, ninaomba nimwulize maswali madogo mawili:-

(i) Kwa kuwa, tabia hii ya kuwasimamisha wasafiri kwenye vichaka kandokando ya barabara kumezaa uchafu mwangi sana wa kupindukia katika maeneo hayo na hasa katika barabara itokayo Mbeya – Dar es Salaam, katika maeneo ya *check point* Makambako na vilevile karibu na njia panda ya Mzumbe, Mkoa wa Morogoro: Je, Serikali iko tayari sasa kufanya au kuchukua hatua za haraka kuyasafisha maeneo hayo ili yaweze kuwa safi kwa usalama wa wasafiri? (*Makofi*)

(ii) Kwa kuwa, maeneo hayo hayana hata huduma ya maji ya kunawa mikono: Je, wakati Serikali inaanda mipango mikubwa ya kujenga vyoo vyenye maji, iko tayari sasa kuweka mipango ya dharura ya kuweka angalau maji ya kunawa ili wasafiri hawa waweze kunawa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu kusafisha maeneo yale yaliyochafuka. Niseme tu kwa hili kwamba ningependa kuchukua nafasi hii kuziagiza Mamlaka za Halmashauri husika kufanya marekebisho hayo na kusafisha maeneo kama ambavyo yameelezwa na Mheshimiwa Hilada Ngoye.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba *SUMATRA* tayari imetoa maelekezo na ratiba ambayo imewapa wasafirishaji wa mabasi husika ili waweze kutumia vituo vilivyoorodheshwa. Wasimame katika vituo hivyo ili wasafiri waweze kupata huduma muhimu pamoja na hii ya kujisaidia.

Katika barabara ambayo Mheshimiwa ameitaja ya Dar es Salaam mpaka Mbeya, kuna vituo kadhaa ambavyo wenye mabasi wanaweza kusimama ikiwemo Morogoro, Mikumi, Kitonga, Iringa, Makambako na Mbeya yenyewe. Kwa hiyo kama mabasi yatasimama katika vituo hivi kama inavyohitajika bila ya shaka tatizo hili la kuchimba dawa ndani ya mapori halitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, kwa mpango wa dharura, hili tutaliangalia na tutalifutilia ili tuone tutaweza kufanya nini ndani ya muda mfupi iwezekanavyo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuzingatie muda. Ni zamu ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, swali linaulizwa na Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama - Mbunge wa Peramiho.

## **Hitaji la Soko la Kimataifa Mpakani mwa Tanzania na Msumbiji**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa Serikali inakamilisha ujenzi wa daraja la eneo la Muhukuru mpakani mwa Tanzania na Msumbiji na kwa kuwa, daraja hilo litafungua biashara nyingi mpakani hapo hali itakayopelekea uhitaji wa soko la Kimatifa na kwa kuwa Halmashauri ilishaomba Serikalini kuwa eneo hilo liwekwe kwenye mpango wa masoko ya Kimataifa na mpaka sasa ombi hilo halijatekelezwa: Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hilo?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista J. Mhagama Mbunge wa Peramiho kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kukamilishwa kwa ujenzi wa daraja ilililoko eneo la Muhukuru litafungua biashara nyingi ambapo hali hiyo itapelekea uhitaji wa soko la Kimataifa. Napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Mbunge, Halmashauri ya Wilaya ya Songea na wananchi wa Songea kwa ujumla kwa hatua waliyofikia ya kuibua mradi wa soko la Kimatifa na kuainisha eneo la kujenga soko hilo.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali kujenga daraja la Muhukuru ni kuimarisha mawasiliano ili kurahisisha shughuli zikiwemo biashara kati ya nchi zetu mbili. Aidha, Wizara yangu ina dhamana kubwa ya kuendeleza masoko na kurasimisha biashara kwa Wilaya zote za mpakani ikiwemo Songea. Mpango wa kujenga masoko ya Kimataifa unatekelezwa kwa kuzingatia vigezo maalum vinavyopatikana baada ya tathmini kufuatia mawasilisho ya uhitaji kama ilivyofanya Halmashauri ya Wilaya ya Songea. Zoezi hili likikamilika Serikali kwa kushirikiana na Wilaya husika watahusika katika kutafuta vyanzo vya rasilimali zinazohitajika yaani (utaalamu na fedha) kutoka nje na ndani ili kuweza kutekeleza mradi huo. Napenda kuwapongeza tena wananchi wa Songea kwa kuwa wabunifu katika kutumia fursa zitakazotokana na daraja la Muhukuru na pia nitoe wito kwao kuanza kuainisha vyanzo vya rasilimali zinazohitajika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuweka mazingira bora ya uwekezaji na kutoa ushauri unaohitajika. Aidha, Wizara yangu iko tayari kutoa ushirikiano utakaohitajika na Halmashauri ya Songea katika zoezi hili kuhakikisha kuwa lengo linafanikishwa.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa daraja hili lililojenga hapo Mhukulu ni daraja ambalo lihna azma ya kuendeleza mashirikiano ya kiurafiki kati ya nchi ya Tanzania na Msumbiji lengo ambalo kwa kweli sasa linafanikiwa na *TAMOFA* chini ya uenyekiti wa

Mheshimiwa George H. Mkuchika, Chama ambacho ni cha urafiti kati ya Tanzania na Msumbiji na mimi kama Makamu wake, Mheshimiwa George H. Mkuchika wa Urafiki huo wa Taifa tumeanza sasa kuona umuhimu wa soko hilo kulipa sifa ya soko la mahusiano ya kiurafiki kati ya nchi hizi mbili. Je, Serikali kupitia Wizara hiyo iko tayari kuwaleta wataalamu kutoka Wizarani kwa kuwa wa kwetu wameshafanya hiyo kazi kuja kuona malengo hayo na kutusaidia kuyafikia na kuyafanikisha kama tulivyofanikisha ujenzi wa daraja hilo?

La pili, kwa kuwa kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo ilikuwa ni kiu kubwa kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho kupitia Mbunge wao na leo daraja hilo limekamilika: Je, Mheshimiwa Waziri atakubali kunisiaidia kumwomba Mheshimiwa Rais aje alifungue daraja hilo yeye mwenyewe ili kuwapa heshima wananchi wa Jimbo la Peramiho kwa kufanikiwa kwa mradi huo muhimu sana kwa nchi yetu kwa kukuza mahusiano kati ya Tanzania na Msumbiji?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumpongeza yeye kama Makamu Mwenyekiti wa TAMOFA na kumpongeza Mwenyekiti George H. Mkuchika kwa kujenga hoja na Serikali kwa kujenga daraja hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwambia kwamba nimekubaliana naye kwamba tutapeleka wataalamu ili waweze kuona namna ya kutekeleza ujenzi wa soko.

Kuhusu swali la pili, hili linahusu Waziri wa Ujenzi na mimi sitasita kushirikiana naye kumwomba Mheshimiwa Rais endapo atakuwa na nafasi bila shaka atakubali.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa, biashara za mipakani ni biashara ambazo zinasaidia sana nchi yetu kuweza kufanya biashara na nchi hizo na kwa kuwa suala la Jimbo la Peramiho ni sawa sawa kabisa na Jimbo la Kalambo katika eneo la mpaka wa Tunduma ambapo Serikali yetu ya Tanzania ndiyo iliyojenga daraja bila kushirikiana na nchi ya Zambia na mahali pale ni mahali ambapo Wizara ya Viwanda na Biashara kwa miaka saba wamekuwa wakiahidi kuwa watajenga soko pale lakini hadi leo hii ninavyozungumza Pasesha hakujajengwa soko lolote, watu wanafanya biashara kwa kutandika vitu chini ambayo ni aibu kwa nchi yetu badala ya kuweza kujenga soko: Je, ni lini Wizara hii nayo itafikiria eneo hili la Pasesha katika Jimbo la Kalambo watajenga soko maana ahadi zimekuwa ni za muda mrefu?

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, Serikali ingependa kuona kwamba kuna masoko katika maeneo yote na katika Wilaya zote za mpakani ikiwemo Wilaya ya Mpanda na eneo la Pasesha.

Mheshimiwa Spika, kama siyo kuwa na uchumi hafifu, basi ungekuta masoko yote hayo yameeshajengwa kwa sababu tunajua kwamba yangeinua biashara kati ya nchi jirani na nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba Wilaya zinazohusika za mpakani ziweze kuibua miradi hii kama ilivyofanya Wilaya ya Songea na ili kushirikiana na Wizara katika kutafuta namna ya kujenga masoko haya hasa katika kutafuta raslimali zitakazowezza kutusaidia kujenga masoko hayo.

Na. 252

### **Kilimo cha Umwagiliaji**

**MHE. ALOYCE B. KIMABO** aliuliza:-

Kwa kuwa, kilimo cha umwagiliaji ni cha uhakika zaidi kwenye maeneo tambarare katika Jimbo la Vunjo katika Kata za Kilema Kusini, Kahe Mashariki, Kahe Magharibi, Mwika Kusini, Makuyuni na Kirua Kusini:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza kilimo cha Umwagiliaji katika Kata hizo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga mabwawa ya maji kwenye Kata hizo?
- (c) Je, matengenezo ya mfereji wa Kimangamau yatakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mbunge wa Vunjo lenye sehemu A, B, na C kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali haipangi mipango ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji kikata. Utaratibu uliopo ni kwa vijiji husika kupendekeza miradi ya umwagiliaji, kuiingia katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) na kuiombea fedha katika *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme ASDP*).

Napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tayari imetenga jumla ya shilingi milioni 315 kupitia Mradi Shirikishi wa Maendeleo ya Kilimo na Uwezeshaji (*Participatory Agricultural Development and Empowerment Project – PADEP*) unaosimamiwa na Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika. Fedha hizi

zitatumika kukarabati miundombinu ya umwagiliaji katika vijiji vya Uchira, Mabungo, Kilema Pofo, Kilototoni, Makuyuni, Lotima, Kyomu, Ngasinyi na Kisangisangeni.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haijawa na mpango wa kujenga mabwawa katika kata alizozitaja Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ya ufinyu wa ardhi katika maeneo hayo ambayo tayari yanakabiliwa na watu. Ujenzi wa mabwawa unataka kuwepo na ardhi ya kutosha kuhifadhi maji. Hili ni tatizo linaloikabili sehemu kubwa ya Wilaya ya Moshi. Kinachotakiwa sasa ni kukarabati na kuboresha mifereji iliyopo ya asili na kuongeza tija katika matumizi ya maji na uzalishaji wa mazao.

(c) Mheshimiwa Spika, tarehe 08 Mei, 2008 kwa mwaliko wa Mheshimiwa Mbunge nilikagua mradi wa uwamgiliaji wa Kimwangamao ambao unahudumia vijiji vya Kinsangisangeni, Mwangiria, Ngasinyi, Mawala na Oria. Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa fedha iliyotolewa na *PADEP*, shilingi milioni 70 itatosha kuendeleza mfereji mkuu tu wenyewe urefu wa kilometra 7.5, lakini kuna haja ya kufanya maombi mapya kwa ajili ya kujenga banio jipya kwenye mto Dehu. Banio la zamani halifai tena kutumika kwa sababu lilijengwa bila utaalami.

Wizara yangu, kupitia Kituo cha Umwagiliaji cha Kanda ya Kilimanjaro inashirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kupima, kusanifu na kukadiria gharama mpya za ujenzi wa banio hilo ili maombi yapitishwe katika Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*DADPs*) na kuombewa fedha katika *Program* ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Programme – ASDP*)

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Katika jibu la Serikali, wamesema kwamba, Serikali haipangi mipango ya umwagiliaji kikata lakini wakati huo huo Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Serikali imetenga shilingi milioni 315 katika kuendeleza mifereji ya Vijiji vya Uchira, Mabungo, Kilema Pofo, Makuyuni, Lotima Kiyomo, Ngasini na Kisangesangeni. Je, Serikali sasa inaweza kusema imetenga kiasi gani cha fedha kwa kila mfereji ili niweze kufuatilia?

Mfereji wa Kimwangamao ni mfereji muhimu sana kwa uhai wa vijiji vya Kisangesangeni, Mwangaria, Ngasini, Mwawala na Oria na kwa kuwa Waziri mwenyewe amekiri banio katika mto Behu linatakiwa kujengwa na katika swali langu la msingi, niliuliza, mfereji wa Kimwangamao utamalizika lini? Je, Waziri anaweza kunihakikishia kwamba atatoa pesa ya kumalizia mfereji huo mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba Serikali imetenga shilingi milioni 315 kupitia Mradi wa *PADEP* na Mheshimiwa anataka kujua kila mfereji umetengewa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, labda kwa suala la kupunguza muda, nimwombe Mheshimiwa Kimaro, baada ya kujibu swali nimpe orodha, maana yake ni ndefu kidogo, itakuwa sio vizuri kuyasoma hapa. Lakini maelezo yapo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la Kimwangamao. Mimi mwenyewe kama nilivyosema, mwezi wa tano nilitembelea mradi huo na nikasikitishwa na jinsi walivyoutekeleza. Niseme tu kwamba, bila kuishirikisha Serikali na hatimaye fedha zilizotumika hazikufa kitu kwa sababu ile kazi yote imekuwa ni ya kurudia. Kwa hiyo, kama nilivyosema, nimeagiza Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji na Halmashauri na hivi sasa wanakamilisha makadirio ya gharama ya kurejesha ule mradi.

Kuhusu ni kiasi gani, naomba asubiri kidogo tutakapokuwa tukiwasilisha hotuba ya bajeti atapata majibu.

**MHE. ESTHERINA J. KILASI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Serikali kwa miaka ya 80 ilipat aufadhili wa *scheme* nyingi za umwagiliaji kwa maana ya miradi ya umwagiliaji kutoka *World Bank, IFAD* na Mashirika mbalimbali ya nje, lakini miradi hiyo haikuweza kukamilika kwa kipindi hicho na iligharimu pesa nyingi sana si chini ya milioni 200 au 300.

Je, Serikali ina mkakati gani sasa ili kuboresha kilimo cha umwagiliaji kupitia miradi hiyo yote ambayo haikuweza kukabidhiwa kwa Serikali kutokana na kutokamilika na mojawapo ikiwa Mbarali. Naomba nijue Serikali ina mkakati gani ili kujua pesa zile hazikupotea bure.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kuliona hili kwa sababu na sisi kama Serikali tumekwishaliona. Tunachokifanya hivi sasa ni kuangalia kila sehemu ambayo tayari ilishafanyiwa upembuzi yakinifu na Serikali imetumia pesa, basi pesa zile zisije zikawa ni kama *sank cost*.

Kwa hiyo, tunaendelea kufanya upekuzi tena kuangalia ni miradi ipi tunawenza kuiendeleza angalau kwa awamu kwa sababu sasa hivi kwamba fedha zinazotakiwa ni nyingi.

Lakini nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Sehemu ile kwa mfano ya Mbarali anayoizungumzia tumejitahidi na hata mwaka huu tutajaribu kuliangalia vizuri zaidi kwamba hata baada ya kutaifisha mashamba yale, yale mashamba ambayo yako nje ambayo yanalinwa na wakulima basi tutayaboresha kusudi waweze kuwa *out growers* wazuri.

**Na. 253**

**Maendeleo ya Miradi ya Maji**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA – kny MHE. KABWE Z. ZITTO aliuliza:-**

Kwa kuwa, Benki ya Dunia ilitoa Fedha za Miradi ya Maji na kila Wilaya ilipewa fungu kwa ajili ya vijiji kumi, ambapo katika Wilaya ya Kigoma Kaskazini vijiji vyta Nkunywe, Kalinzi na Nyambande vilifaidika: Je, nini maendeleo ya miradi hii?

#### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mbunge wa Kigoma Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeandaa programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji ya mwaka 2006-2025. Programu hiyo ina programu ndogo nne, ikiwa ni pamoja na programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Programu ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini inatekelezwa katika Halmashauri zote nchini ikiwa na lengo la kuwapatia wananchi maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mpango wa utekelezaji wa programu ni kuwa katika hatua ya kwanza kila Halmashauri imechagua vijiji 10 ambavyo utekelezaji wa programu utaanzia. Katika Halmashauri ya Kigoma Vijijini, vijiji 10 vilivyochaguliwa ni Ilagala, Kandaga, Uvinza, Nguruka, Kalya, Rukoma, Kagongo, Nyarubanda, Nkungwe na Kalinzi.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi katika vijiji 10 vilivyotajwa kwa muda mrefu umekuwa unasuasua kutoana na ugumu wa masharti ya manunuzi ya Benki ya Dunia. Hadi mwezi Septemba, 2007, Halmashauri sita tu za Arusha, Kasulu, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Moshi, Rombo na Manispaa ya Temeke ndizo zilizotimiza kikamilifu masharti yote.

Kwa kutambua kuwa Halmashauri nyingi hazikuwa na uwezo wa kutekeleza matakwa ya Benki ya Dunia katika taratibu za manunuzi, Serikali iliomba Benki ya Dunia kulegeza masharti yake. Tarehe 8 Julai, 2008 kama mlivyo sikiya Benki ilikubali kulegeza masharti yake ambapo Halmashauri 82 ikiwemo Kigoma Vijijini sasa zimeruhusiwa kuendelea na utaratibu wa kupata kampuni zitakazoandaa mapendelekezo ya usanifu wa miradi ya maji. Wakati tunasubiri kuanza kwa programu nzima, Serikali ilianzisha utaratibu wa kutoa fedha za kukarabati miradi ya maji inayotekelzeza na kutoa matokeo haraka, maarufu kama *Quickwins*. Kwa bahati mbaya kwa miaka miwili mfululizo, 2006/2007 na 2007/2008 Halmashauri ya Kigoma Vijijini haikufuzu kupata fedha za ruzuku ambazo zingeweza kuhudumia baadhi ya vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge. Hata hivyo, kwa bahati nzuri, mwaka 2008/2009, Halmashauri hiyo imefuzu kupata fedha za ruzuku.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa sasa Benki ya Dunia imelegeza masharti yake na kwa bahati nzuri Halmashauri ya Kigoma vijijini nayo imefuzu kupata fedha hizo. Ni lini fedha hizo zitatolewa na ni lini mradi huo utaanza na kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya nikiwa na furaha kwa sababu na mimi ni mdau wa suala hili kwamba sasa kwa sababu Benki ya Dunia imelegeza maana yake ni kwamba hicho ni kiashiria kwamba sasa endeleeni na mchakato. Kwa maana hiyo ni kwamba kazi imebaki kubwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma Vijijini kuendelea na mchakato huo kwa sababu jinsi tutakavyofanya mchakato na kuendeleza haraka ndivyo tutakavyopata hizo pesa.

Tungependa tu kwamba angalau mchakato huo basi ifikapo mwezi wa tatu mwakani uwe umekwishakamilika ili kazi za utekelezaji halisi ziweze kuendelea.

Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba na mimi nitamsaidia Mheshimiwa Zitto na Mheshimira Ruhwanya kuhakikisha kwamba Halmashauri ile inakamilisha kazi hizi. (*Makofi*)

Na. 254

#### **Msomganamo wa Wafungwa na kuenea kwa VVU**

##### **MHE. DK. ALI TARAB ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna msongamano mkubwa wa wafungwa katika Magereza yetu hapa nchini:-

- (a) Je, msongamano huo huathiri kwa hali yoyote kusambaa kwa VVU/UKIMWI?
- (b) Je, kuna utafiti wowote ulifanyika kujua kiwango cha VVU/UKIMWI katika Magereza hapa nchini?
- (c) Kama umefanyika, je, kiwango hicho kikoje?

##### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Ali Taarab Ali Mbunge wa Konde lenye sehemu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, wafungwa na mahabusu ni jamii kama zilivyo jamii nyingine na uwepo wao Magerezani ni kwa mujibu wa Sheria za nchi. Hivyo wana fursa sawa ya kupata taarifa na elimu sahihi ya Virusi vya UKIMWI na Maambuzi yake kama jamii nyingine zilizo nje ya Magereza.
- (b) Mheshimiwa Spika, Msongamano wa Wafungwa hauchochei kasi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI katika Magereza yetu. Usambaaji wa VVU/UKIMWI katika Magereza yetu unadhibitiwa kuitia mikakati na taratibu maalum zilizowekwa na Jeshi la Magereza ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya VVU/UKIMWI kuitia mabaraza ya wafungwa, uwepo wa usimamizi baina ya wafungwa wenyewe ndani ya mabweni,

vipindi nya redio, TV, sana hasa nyimbo na maigizo, mabango na vipeperushi na pia kuhakikisha kila mfungwa anatumia kifaa chake alichopewa kwa ajili ya kunyolea na kukatia kucha.

(c) Mheshimiwa Spika, hakuna utafiti uliofanyika kujuu kiwango cha VVU/UKIMWI Magwerezani. Hata hivyo, mnamo mwaka 2006 Jeshi la Magereza baada ya kuwahamasisha Wafungwa juu ya umuhimu wa kupima afya zao jumla ya wafungwa 3,556 walijitolewa kupima kwa hiari. Lengo la umasishaji huu ilikuwa ni kuweza kuona kiwango cha VVU/UKIMWI katika Magereza yake hapa nchini.

(d) Mheshimiwa Spika, matokeo ya upimaji huo wa hiari uliofanyika mwaka 2006 ulihusisha jumla ya wafungwa 3,556, kati ya hao wafungwa 327 ambaa ni sawa na 9.2% walipatikana na VVU/UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu ikaelewaka kwamba suala la kupima VVU/UKIMWI kwa mfungwa ni suala la hiari. Hivyo, sio rahisi kupata kiwango sahihi cha maambukizi au waathirika waliopo Magerezani. Napenda kuchukua fursa hii kuwaomba wafungwa waliopo Magerezani waone umuhimu wa kujuu afya zao kwa kuamua kwa hiari zao kupima UKIMWI. Aidha, Serikali itakuwa tayari kutoa huduma maalum kwa waathirika ili waweze kuishi kwa muda mrefu wakiwa na afya njema.

**MHE. DK. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kiwango cha 9.2% kiko juu ukilinganisha na 7% ambayo ilikuwa ni wastani kwa mwaka huu wa 2006. Wafungwa ni wanadamu na kama ni wanadamu pia wana matamanio na kwa vile ni wafungwa wa jinsia moja wanawekwa katika bweni moja: Je, huu usimamizi wa wafungwa wenye kwenye mabweni unafanyika kwa makini?

La pili, je, wale wanaougunduliwa kwamba wana virusi nya UKIMWI wanapata lishe nzuri na dawa za kupunguza makali ya virusi nya UKIMWI?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi ndani ya Magereza, usimamizi tunaoufanya ni makini na jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba umakini unakuwepo zaidi na ukitizama kwa kweli nafikiri ingawaje kweli amesema kwamba *National Average* ni 7.2 na ile ya Gereza ni kubwa kidogo lakini pia nafikiri Dk. Tarab anavyoolewa ni kiasi cha kutumia kutazama *base statistics* ambazo zimetumika.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ile *base* ya wafungwa inakuwa ni ndogo zaidi kuliko ile ya Taifa kwa ujumla.

Lakini hivyo kwa kujibu swal lako ni kwamba jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba usimamizi unakuwa ni wa makini. Lakini hatuna njia nyingine maana yake wafungwa wa jinsia moja itabidi wawe wa jinsia moja na ndivyo ilivyo sio hapa Tanzania, lakini Magereza yote ulimwengu mzima.

Kuhusu swali la pili, jitihada zinafanyika kuhakikisha kwamba wafungwa wanapata chakula na lishe iliyo bora na wanapata madawa yaliyokuwa bora.

Mheshimiwa Spika, Kitu kimoja ningependa nihimize tu kwamba mtu kufungwa haijamwondolea ubinadamu wake wala hajampunguzia haki zake za msingi kama Mtanzania au kama binadamu. Ni kwamba tu amefanya kosa, atakuwa katika adhabu ya kosa alilolifanya lakini utu wake, Utanzania wake na shughuli ambazo anapaswa kupata huduma kutoka katika Serikali zinabaki pale pale.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ingawa muda wa maswali sasa umefika kikomo, lakini nadhani ni utaratibu mzuri tuyamalize haya maswali ya Wizara ya Nishati na Madini.

Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina wa Geita.

Na. 255

### **Kuongeza *Transfoma* Kwenye Mji Mdogo wa Kasamwa**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Kasamwa ulipatiwa umeme mwaka 2004 kwa kutumia mradi maalum ambapo *transfoma* moja iliwekwa kutumika kwenye *ginnery* ya pamba na moja kwa matumizi ya wananchi na kwa kuwa hiyo *transfoma* moja haitoshelezi mahitaji ya wananchi hao:-

Je, Serikali itaongeza *transfoma* nyingine ili kukidhi mahitaji ya Kituo cha Afya, Shule ya Sekondari Kasamwa, Kituo cha Maaskofu Kasamwa na wananchi kwa ujumla?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mji mdogo wa Kasamwa ulipata umeme mwaka 2004 ambapo *transfoma* mbili ziliwekwa, moja kwenye kinu cha kuchambulia pamba na nyingine kwenye Mji mdogo kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Mji huo. *Transfoma* iliyowekwa kwa ajili ya kusambaza umeme kwa wananchi haitoshelezi mahitaji ya Mji huo mdogo na Vitongoji vyake.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo, *TANESCO* inafanya juhudhi mahsusini kuongeza *transfoma* nyingine mbili zitakazosambaza umeme kwenye maeneo hayo kwa matumizi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa 2008, Shirika la Umeme (*TANESCO*) limetenga Shilingi milioni 21.8 kwa ajili ya uwekaji wa *transfoma* moja ya 100 KVA na ujenzi wa njia ya kusambaza umeme ya msongo wa 0.4 KV yenye urefu wa kilomita moja. Lengo likiwa ni kupeleka umeme kwenye Kituo cha Afya cha Kasamwa na nyumba za wafanyakazi wa kituo hicho. Kazi hii inatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka huu 2008.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Umeme (*TANESCO*) linatarajia kutenga kiasi cha Shilingi milioni 75 katika bajeti yake ya mwaka 2009 kwa ajili ya awamu ya pili, ambayo itahusisha uwekaji wa *transfoma* mbili za 100KVA na ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa 0.4KV yenye urefu wa kilomita tano kuelekea Kasamwa Sekondari, Kasamwa *Mission* na maeneo ya jirani. Awamu hii inatarajiwa kuwafikia wateja wa umeme 220. Kwa hiyo, tunawaomba wananchi wa Kasamwa wawe wavumilivu wakati Serikali ikifanya jitihada za kukamilisha mradi huu.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Serikali katika miradi hii ya umeme inakubali tu kiurahisi na katika mradi huu wa Kasamwa ni mradi mdogo sana kiasi ambacho naona Serikali imetenga mara mbili, kwa nini isifanye mara moja tu tukaondokana na tatizo la umeme katika Mji wa Kasamwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kusema kwamba Serikali haikubali kirahisi rahisi tu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge angependa iaminike au ielevweke, hapana. Serikali inawatumikia wananchi wake, inatoa taarifa kwa jinsi ambavyo miradi inatekelezwa kulingana na uwezo wa fedha ulivyo. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Geita kwamba, sio Serikali inakubali kirahisi hapana! Tunachokisema ni sahihi! Fedha imeshatengwa na tunafahamu kwamba pale Geita zinahitajika zaidi ya *transfoma* tatu na *TANESCO* itatenga shilingi milioni 785 kukamilisha mpango huo wa usambazaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, hii sio hadithi, ni ukweli kwa sababu mwaka wa fedha wa *TANESCO* ni *calendar year* kwamba unaanza Januari, 2009 hauendani na *financial year* kama ilivyokuwa kwenye utaratibu wa kawaida unaanza mwezi wa Saba. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kwamba, inachosema Serikali inakimaanisha kwa dhati.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza kabisa pamoja na shukrani nyingi sana kutoka kwa wananchi wa Mbanga kwa maendeleo ya umeme yanayoendelea, tunaomba pia kufikisha ujumbe kutoka kwao, kutokana na hali ya sasa kwamba wanatumia mita za *LUKU* ambazo haziwezi kununuliwa umeme wake siku za Jumamosi na Jumapili: Je, Mheshimiwa Waziri

ataweza kuwasaidia ili wapate huduma hiyo angalau kwa kuweka *vending station* moja?  
(*Makofii*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, tunapokea ushauri wake na tutawasiliana na wataalam wetu ili tuone jinsi ya kutengeneza rai yake. Ahsante.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kuuliza swali langu, kwa kuwa Mheshimiwa Savelina Mwijage ni Naibu Kivuli wangu na kwa kuwa amepata msiba mkubwa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mkanyageni ambao wanamfahamu sana Mheshimiwa Savelina, natoa pole kwa msiba uliotokea wa mtoto wake Stella na dereva wake, Mwenyezi Mungu ampe subira na azilaze roho za Marehemu Peponi na ampe uvumilivu na tupo pamoja naye katika kipindi hiki kigumu.

Na. 256

### **Madini Kutokuwa Suala la Muungano**

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali wakati ikijibu swali Na. 427 kwenye Mkutano wa Nane wa Bunge ilisema kuwa Maliasili ya Madini sio suala la Muungano na kwa kuwa Maliasili Mafuta na Gesi ni masuala ya Muungano:-

- (a) Je, ni vigezo gani vilivyofanya Maliasili Madini isiwe ya Muungano, lakini Mafuta na Gesi vikawa vya Muungano?
- (b) Je, kuanzia tarehe gani na mwaka gani Mafuta na Gesi yamekuwa ya Muungano?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Habib Juma Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Nane, Kikao cha 46 cha Bunge lako Tukufu wakati wa kujibu swali Na. 427 la Mheshimiwa Ame Pandu Ame, ilielezwa kuwa Maliasili Madini sio za Muungano, isipokuwa Maliasili Nishati zinazohusisha Mafuta na Gesi ni za Muungano. Kigezo kilichofanya Maliasili Madini isiwe ya Muungano, lakini Mafuta na Gesi vikawa vya Muungano ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Ibara ya nne na Nyongeza ya Kwanza) ambayo ndiyo inayotoa mwongozo na sheria zote za nchi zinifuata Katiba.

Mheshimiwa Spika, shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi hutekelezwa chini ya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Mafuta ya Mwaka 1980 [*Petroleum (Exploration and Production) Act, 1980*]

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kwa sasa Maliasili Madini sio ya Muungano, lakini mapato yanayotokana na madini yanakwenda moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Mapato ya Serikali ambao ndio unagharamia uendeshaji wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.

(b) Mheshimiwa Spika, Maliasili ya Mafuta na Gesi imekuwa ya Muungano tangu katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipotungwa na kubainisha mambo yapi ni ya Muungano na yapi sio ya Muungano.

**MHE. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Spika, nina swalii moja tu la nyongeza. Kwa kuwa vigezo viliviyotumika ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kuwa Katiba hii imeonyesha utata mpaka ikapelekeea Mheshimiwa Waziri kuagiza Wanasheria wa pande mbili wakutane kuhusu suala la Zanzibar kuwa nchi au siyo nchi, kwa kuwa Serikali imetafuta Mshauri Mwelekezi kutoka Kampuni ya APGUM kuhusu utata huu wa mafuta na gesi; vilevile katika jibu la Waziri amezungumzia Ibara ya (4) ambayo haitoi ufanuzi wowote kuhusu mafuta na gesi isipokuwa inazungumzia mamlaka ya vyombo vyenye kutoa haki kama Baraza la Wawakilishi na Mahakama: Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kutoa tamko katika Bunge kwamba, kwa vile Katiba ina utata, hao Wanasheria watakapokutana kutafsiri mambo tofauti ya Katiba ili kipengele hiki cha mafuta na gesi wakizungumzie, aidha, kwamba itolewe katika Muungano, mafuta na gesi au madini nayo yaingizwe kuwa ni ya Muungano? (*Makofi*)

**SPIKA:** Nadhani hili halimo katika mamlaka ya Waziri mhusika kwa sababu agenda za vikao vya pamoja zinasimamiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais. (*Makofi*)

Waheshimiwa muda wa maswali umekwisha na sasa ni wakati wa matangazo. Kabla sijayasoma, kama mnavyofahamu, nilipokuwa safarini Zambia, kulitokea misiba hapa. Nami naomba niungane nanyi nyote kuwapa pole wenzetu ambao wamepatwa na misiba, hususan Mheshimiwa Savelina Mwijage aliyefiwa na mwanawewe, lakini pia Mheshimiwa Naibu Spika, ambaye alifiwa na dada yake ambaye amezikwa jana kule Kongwa na ndiyo maana hayupo hapa. Nami pia naungana nanyi wote kumwombwa Mungu awalaze mahali pema Marehemu hao.

Wale ambao bado wanaugua, majeruhi pia tunawaombea wapate afueni ili waweze kuungana na jamii katika shughuli mbalimbali na wafiwa tunaomba wawe na moyo wa ujasiri au imara katika wakati huu. Hii ndiyo mitihani ya Mwenyezi Mungu na sote lazima tutapitia hayo.

Nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Wabunge wenzangu tuliokwenda pamoja Zambia, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Zainab Vulu na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, wawili bado wamebaki huko kwa sababu mimi nimewahi ili kuwahi shughuli. Napenda kuwahakikishieni Waheshimiwa Wabunge kwamba Wabunge hawa wametuwalisha vizuri sana, tumeacha jina zuri sana kule CPA Zambia.

Sasa ni matangazo. Kwanza kuna wageni wa Mheshimiwa Waziri Profesa Juma Kapuya, mkewe bibi Tatu Kapuya nadhani yuko pale. Wanawe Kulwa na Cosmas Lomano, wale pale. Yupo pia Yasin Omar Masebu ambaye ni Katibu wa Mbunge Jimbo la Urambo Magharibi. Karibu sana Sheikh Yasin. Yupo Ibrahim Maganga, mgeni kutoka Jimboni na pia wapo wanafamilia Bw. Ali Mapinda na Mzuri Kapuya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Kwa Mheshimiwa Waziri, wapo pia watendaji kutoka Wizarani ambaa ni Katibu Mkuu - Dr. Komba; Bibi Mangesho - Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kazi na naomba Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi wa Wizara ya Kazi nao wasimame kwa pamoja. Karibuni sana.

Wapo pia Viongozi wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kazi ambaa ni Mwakilishi wa *ILO* - Bibi Deborah Nyakilang'anyi; Dr. Kassim Kapalata - Kaimu Mwenyekiti wa Usuluhishi na Uamuzi; Ndugu Kitumbo - Mkurugenzi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (*OSHA*); Ndugu Mwasele, Mtendaji Mkuu, Wakala wa Huduma ya Ajira; Ndugu Mkakatisi, Katibu Mkuu *TUICO* na Mjumbe wa Bodi ya *NSSF*; Dr. Ramadhani Dau, Mkurugenzi Mkuu wa *NSSF*; huyu bwana maarufu sana. *NSSF* sijui ni lini itawekeza Urambo. Inawekeza kote kwingine ila Urambo tu. (*Makofi/Kicheko*)

Pia kuna Ndugu Mrosso - Mkurugenzi wa Fedha *NSSF* na Ndugu Kigula - Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji, *NSSF*. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia Mwenyekiti wa Chama cha Waajiri (*ATE*) - Ndugu Mbwanji, naona hayupo, wapo ndugu Kingazi na Ndugu Mgaya - Wajumbe wa Bodi ya *NSSF*. Yupo ndugu Nestor Ngulla - Katibu Mkuu wa *TUCTA*, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi, karibu sana ndugu Ngulla. Ndugu Mtari - Mwenyekiti wa Shirika la *TIJA* na ndugu Kasenge - Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la *TIJA*. (*Makofi*)

Wapo na wengine ambaa ni kikundi cha wajasiriamali kutoka Dar es Salam ambaa wamealikwa na Mheshimiwa Waziri, ningeomba kwa pamoja wasimame. Ni akina Rweyemamu, Nyamiti, Ziota, Makaranga, Tarimo, Kakoo na Vaileth Kapuhilwa, karibuni sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nina wageni wangu pia, wapo *Speaker's Gallery* wakiongozwa na binamu yangu ambaye baada ya mchakato, amechaguliwa kuwa Chifu wa

Wanyanyembe - Chifu Msagata Ngulati Fundikira. Yule pale amevaa vazi la jadi, akiwa na mkewe ambaye kwa lugha yetu anaitwa Mgoli - Mwamvita Fundikira, yule pale. Katika utaratibu wetu kule nyumbani tulianza nadhani kabla ya Wazungu kuwa na Waziri Mkuu, pale Ikulu, hata neno Ikulu mnajua linatoka huko huko. Ndugu Mwelekeza Omar Fundikira, ndiye Waziri Mkuu pale Itetemya; Bwana Juma Ibrahim, Mtemi wa Waswezi. Karibuni sana. (*Makofi*)

Chifu huwa ana makandokando, anaandalisha mazingira fulani, kwa hiyo, anakuwa na Waswezi, ni wataalam wa mambo ya jadi na wanasaidia pia katika

uhamasishaji wa ngoma za aina mbalimbali na wanafuatana na binamu yangu mwingine Bwana Juma Abdallah Fundikira, ambaye ye ye ni Mwanangwa. Nami pia ni Mwanangwa (*Prince*). (*Kicheko/Makofi*)

Najua kumekuwa na watu wanahoji na mambo ya migogoro siku hizi kuhusu Uchifu huo, lakini tunadhani mambo yatakwenda vizuri ili wathibitishwe rasmi. Karibuni sana.

Kuna wageni wa Mheshimiwa Michael Laizer amba o ni Mheshimiwa Thabit Ole-Matipets, mwanafunzi wa Chuo KIkuu Mzumbe. Karibu sana. (*Makofi*)

Pia kuna wageni wa Mheshimiwa Nimrod Mkono amba o ni Bwana Calvis Bagets kutoka Oklahoma, USA. *Our visitor kutoka USA, Oklahoma State, there he is. You are warmly welcome Sir. Welcome to a Parliament of Tanzania, together with Barbra Waterston, thank you very much. We are happy to see you. We want to encourage visitors to visit peaceful Tanzania. I am sure you are very safe and in hands of the distinguished honourable Mkono, you are even safer. Thank you. (Applause)*

Tuna Viongozi wawili kutoka Asasi isiyo ya Kiserikali ya akinamama wajane inaitwa ‘Y’ for Widows Forum Foundation, amba o ni ndugu Josephine Mahimbo na ndugu Mary John Lyimo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Pia tuna wanafunzi hamsini na Walimu wanne kutoka shule ya Msingi Valentine, nadhani hawakupata nafasi. Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Msingi Kizota, Dodoma, nao hawapo. Kuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari Kikuyu, nadhani wale pale pamoja na Walimu wao, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia Viongozi 25 vya Shirikisho la Vyama vya Walema vu Tanzania, wale pale wananyoosha mkono. Ahsante sana, tunashukuru kwa jitihada mliyochukua kuweza kufika hadi hapa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naitisha kikao kifupi cha Kamati ya Uongozi, *Steering Committee* na Tume ya Huduma za Bunge saa saba katika Ukumbi wa Spika. Naomba Wajumbe wote tukutane ni kwa muda mfupi.

Baada ya hapo, Mheshimiwa Lubeleje ambaye ni mshiriki kwenye kikao changu, anaomba wale wote wa Kamati Ndogo ya Uongozi na Tume wanaoshughulikia suala la *CDF* na Muswada wetu wa *National Administration Bill* wakutane mara baada ya mkutano, nadhani saa 7.30 ukumbi wa Pius Msekwa. Tunataka mambo yaharakishwe yaweze kwisha ili tufanye mambo mengine ya maana. Kwa hiyo, mkutano kuhusu *CDF* na Muswada wa Sheria ya Utawala ya Bunge ni saa 7.30 katika ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Waziri Profesa Juma Kapuya ameniomba nitangaze kwamba yapo maonyesho ya nguvukazi Juakali ambayo yanaendelea tangu tarehe 18 - 23 Julai, 2008 kwenye viwanja pale. Haya maonyesho ni sehemu ya maandalizi ya ushiriki wa

wajasiriamali wetu katika maonyesha ya Nguvukazi Juakali yatakayofanyika Kigali, Rwanda tarehe 29 Novemba – 2 Desemba.

Waheshimiwa Wabunge, tuwatie moyo wajasiriamali wetu hawa kwa kuhuduria, kuwahamasisha na kuwapa ushauri. Kwa hiyo, Waziri anatoa fursa kwamba tuwatemelee na tuwape nguvu ili wakienda huko Kigali waweze kufanya kazi nzuri zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, huo ndio mwisho wa matangazo na sasa nitamwita Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

(*Majadiliano yanaendelea*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Spika, mgogoro wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari, *TPC* Moshi ni mgogoro unaodumu takriban miaka mitano sasa, tokea ulipoibuka mwaka 2003 pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na wahusika hasa wafanyakazi kutafuta suluhisho.

Mgogoro unahusisha wafanyakazi 168 waliofukuzwa kazi tarehe 24 Februari, 2008 na wafanyakazi wengine zaidi ya 2,300 ambao wapo kazini, lakini pia wanaohusika na wana madai ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mgogoro unalenga juu ya haki ya kisheria ya wafanyakazi kujiunga na kuwa sehemu ya chama huru cha wafanyakazi ambapo kwa njia moja ama nyingine haki hii inaonekana kukataliwa au kunyimwa na uongozi wa kiwanda pamoja na Serikali kwa jinsi hali ya mgogoro huu inavyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi walikikataa chama cha wafanyakazi cha *TPAWU* ambacho hakikuwa na ufanisi na nguvu katika kufuatilia maslahi, kushughulikia na kutatua matatizo ya wafanyakazi hao hali iliyopelekea kujiunga na *TUICO*. Pamoja na hatua hii, walioichukua *TUKTA* ikishirikiana na uongozi wa kiwanda pamoja na msajili wa vyama vya wafanyakazi walizua *TUICO* kuwahudumia wafanyakazi hawa au kuwa sehemu ya chama hicho. Wafanyakazi hao kwa kuonyesha msimamo wao wa kutoitaka *TPAWU* walichukua hatua ya kujiunga na chama kingine cha wafanyakazi cha *TASIWU*. Bado hatua hii haikuwasaidia, kwani *TASIWU* nayo haijaruhusiwa kuwahudumia pamoja na kukamilisha masharti ya kubadilisha Katiba yake ili iwe na uwezo wa kuwasajili wafanyakazi hawa.

Kufukuzwa kazini wafanyakazi 164 pamoja na viongozi wao wanne ni kwa sababu walijaribu kuulizia mustakabali wa fedha zao za ada zilizokuwa chini ya ulinzi wa Mahakama ambazo zilizuiwa kupelekwa *TPAWU* au *TUICO* lakini uongozi wa *TPC* ukaenda kinyume na amri hiyo na kuzipeleka fedha zote *TPAWU*.

Kufukuzwa viongozi wanne, wafanyakazi hao, kwa sababu ya kuongea kupitia *Star TV* siku ya tarehe 7 Januari, 2008 wakiitaka Serikali iingilie kati mgogoro huu, hii ilipelekeea mwajiri kuchukua hatua ya kuwafukuza wafanyakazi wafuatao isivyo halali.

- (1) Menace Gidioni
- (2) Justine Samwel
- (3) Meliki Mwerinde
- (4) Sarapia Mmasi

Mheshimiwa Spika, manyanyaso yanayotokana na mgogoro huu kwa wafanyakazi, Uongozi wa Kiwanda unawabambikiza kesi kama vile za wizi wa miwa ambazo ziko katika Mahakama ya Mkoa na Wilaya Moshi. Pia uongozi unajigamba kwamba ni lazima wafanyakazi hawa watafungwa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya Wafanyakazi hawa kwa Serikali ni kama ifuatavyo:-

(1) Chama cha Wafanyakazi cha *TASIWU* kiruhusiwe kufanya kazi kwa haraka kwani ni chama halali chini ya sheria ya kazi Na. 6 ya mwaka 2004;

(2) Serikali iwakutanishe wafanyakazi 168 na uongozi wa kiwanda *TPC* kutatua mgogoro huu badala ya kuiachia Mahakama ambayo itachukua muda mrefu wakati wafanyakazi, walalahoi wanaendelea kuumia na kimsingi wafanyakazi hawa warudishwe kazini;

(3) Kwa kuwa mgogoro huu unahu wafanyakazi kujiunga na chama huru cha wafanyakazi lakini inaonekana kuna mizengwe na hii sio kawa, tunaomba Mheshimiwa Waziri mhusika aunde Tume maalum kuchunguza sababu za haya yote na tuko tayari kushirikiana nayo;

(4) Serikali ihakikishe sheria za kazi zinafuatwa na haki za wafanyakazi zinalindwa; na

(5) Serikali ifuatilie maslahi ya wafanyakazi wazalendo na hali halisi ya wafanyakazi hao katika sekta binafsi na iache kuwapendelea wawekezaji kutoka nje.

**MHE. SAID ARFI:** Mheshimiwa Spika, vijana ni kundi kubwa katika nchi yetu na nguzo ya ustawi wa Taifa lolote kama wataendelezwa. Lakini vijana wa nchi hii hawana mahali pa kuzungumzia pamoja na kwamba vijana, isipokuwa vijana hawa wamegawanywa katika vikundi vidogo vidogo vya kiiitikadi za kisiasa zaidi, jambo ambalo mimi nadhani kwa mtazamo wangu linawanyima fursa vijana ambaao hawajawa tayari kujiunga katika vikundi hivyo vya kiiitikadi kuweza kutoa michango yao ya kifikra

katika nyanja mbalimbali ili kuweza kuleta mabadiliko na maendeleo yao na nchi kupitia jukwaa moja la Baraza la Vijana.

Mheshimiwa Spika jambo hili vijana wenyewe wamekuwa wakilihitaji, nadhani ipo haja ahadi iliyotolewa muda mrefu juu ya jambo hili iwe imetekelozwa.

Mheshimiwa Spika, dhamira njema ya Mheshimiwa Rais ya kupeleka shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa, sidhani kama tija iliyokusudiwa imepatikana na kuwanufaisha walengwa waliokusudiwa. Ni vyema basi, sasa tukapewa tathmini ya mafanikio yake na mapungufu maana hivi majuzi tu Mheshimiwa Rais ameagiza wale waliokopeshwa warejeshe mikopo yao kwa maana mfuko huo au pesa hizo ni za mzunguko. Wale ambao watakuwa wameshindwa kurejesha wanachukuliwa hatua gani? Je, hatua zitakazochukuliwa zilikuwa zimeainishwa katika mikataba ya mikopo ile?

Mheshimiwa Spika, nitapenda kujua hasa, wanawake wangapi wamefaidika katika Wilaya ya Mpanda na maeneo ambayo mikopo hiyo imetolewa na kama hakuna mikopo iliyotolewa ni kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, hali ambayo sasa inajitokeza nchini, ni migomo ya wafanyakazi na hiyo ni silaha halali ya wafanyakazi, baada ya majadiliano ya awali kutotoa majawabu, lakini kwa jeuri ya waajiri wa leo ambao wanabebwa na masharti ya hovyo ya uwekezaji, watumishi hawa wanafukuzwa kazi na Wizara inakaa kimya. Hii maana yake nini? Wizara inapaswa kwanza kuangalia maslahi ya Watanzania ambao kwa kura zao wamewapa dhamana ya kusimamia maslahi yao, hivyo basi, Wizara inapaswa sasa kujikita katika kujenga mahusiano mazuri kati ya waajiri na wafanyakazi kwa maslahi ya nchi na ina kuepusha migomo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, wakati nachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilitoa malalamiko yangu juu ya Serikali (Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana) kwamba:-

(1) Kwa kutambua kuwa Jimbo la Nyang'hwale halikupata mgao wa awamu ya kwanza ya fedha za Wajasiriamali (pamoja na ukweli kuwa Wilaya ya Geita ni moja ya Wilaya zilizopata mkopo mkubwa zaidi ya Daraja 'A');

(2) Katika Bunge hili, Wizara imeahidi mara mbili (wakati ikijibu maswali yangu) kuwa awamu ya pili Jimbo la Nyang'hwale litapatiwa mgao huo, kwani halikupata katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba maelezo ya kiasi gani na ni lini wajasiriamali wa Jimbo langu watapata ahadi yao kwani awamu wa pili tayari kuna maeneo wameanza kupatiwa.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya

Vijana - Mheshimiwa Profesa Juma Kapuya, Naibu Waziri - Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki kundaa bajeti hii nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha tija katika Wizara hii, ninawaombea Mungu awape afya, nguvu na moyo wa kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya pungezi sasa nianze kuchangia kama ifuatavyo:- Kupitia ilani ya uchaguzi ya mwaka 2005 – 2010, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete katika mambo mengi aliyohidi kutekeleza ni pamoja na ajira kwa vijana. Je, ni vijana wangapi hadi leo wamepata ajira kwa kuajiri au kuajiriwa? Kwa kuwa wimbi la vijana bado ni kubwa sana ambao hawana ajira na sifa wanazo, mfano waliomaliza elimu darasa la saba, kidato cha nne, *Diploma* na Chuo Kikuu. Ninapenda kujua Serikali ina mpango gani kupitia bajeti hii? Naomba Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho anipe maelezo.

Mheshimiwa Spika, ninatambua Serikali inafahamu kuwa kuna wimbi kubwa sana la vijana ambao wamejihuisha na utumiaji wa madawa ya kulevyta na kwa kuwa vijana kuzagaa kwao Mitaani ni aibu kwa Taifa na ni kero kwenye familia wanazotoka na raia wengi kwa ujumla, ninaiomba Serikali kujenga vituo vya kuwalea vijana hawa pamoja na kuwafundisha kazi mbalimbali za uzalishaji mali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Ufundji pamoja na Wizara ya Afya. Nina hakika mkakati huu utasaidia kuondoa wimbi kubwa la vijana pia kusaidia kubadili tabia zao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa migogoro kazini mingi hutokana na waajiri wengi kutowatimizia wafanyakazi haki zao: Mfano, wafanyakazi kutokupata mishahara kwa wakati, kutokulipa madai ya wafanyakazi mapema, kupanda madaraja pale wanapostahili na mengine mengi, napenda kujua mkakati wa Wizara hii ili kuepuka kabisa migogoro ya wafanyakazi na waajiri wao. Nasubiri maelezo ya Mheshimiwa Waziri pamoja na wafanyakazi kusimamishwa kazi bila ya kufuata taratibu za ajira.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kutoa mikopo kwa vijana kupitia *CRDB* na *NMB* kwa ajili ya kutunisha mifuko yao kwa lengo la kuboresha miradi yao ya maendeleo kwa vijana wenye nia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuijulisha Serikali kuwa, utoaji wa mikopo hii haitoi huduma kwa vijana walioko vijijini, ninaiomba Serikali sasa huduma hii ielekezwe vijijini ili vijana wengi wajasiliamali waweze kufaidi matunda ya Serikali yao kwa lengo la kuondokana na umaskini vile vile mikopo hii inayopitia benki ina usiri mkubwa sana, suala ambalo viongozi tunashindwa kufahamu hamasa tunayotoa inazaa matunda kiasi gani. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua jitihada zinazofanywa na vyama vya wafanyakazi katika kutolea haki na maslahi ya wafanyakazi wote walioko Serikalini na sekta binafsi. Ili kujenga umoja, mshikamano na ufanisi kazini, napenda kujua Wizara huwa ina utaratibu gani wa kukutana na vyama hivi ili kuimarisha mshikamano wa vyama hivi na Serikali. Nitashukuru endapo Mheshimiwa Waziri atatoa maelezo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kusaidia vijana katika harakati za kuondokana na umaskini. Napenda kufahamu Mfuko huu, Wizara huwa inachangia asilimia ngapi na vile vile nielezwe mpango huu bado unaendelea na Halmashauri huwa zinachangia asilimia ngapi katika Mfuko huu wa Vijana?

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kuendeleza Mfuko huu ambao umekuwa msaada sana kwa vijana, kwani sasa hivi wana mwamko sana na harakati za kuondokana na umaskini. Vile vile utoaji wa mikopo hii itolewe kwa haki wakishirikisha vijana wote hadi vijijini.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa kutambua jitihada nzuri zinazofanywa na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF - ndugu Dau kwa kazi kubwa anayofanya kujenga majengo mbalimbali kwa kukopesha Taasisi za Serikali na binafsi kwa lengo la kuleta maendeleo na kuondoa kero ya nyumba za kuishi, ofisi, shule, vyuo na biashara. Ninashauri shirika hili la NSSF kuongeza huduma hii kwa kujenga majengo haya hadi Mikoani. Ninawakaribisha pia Singida, kwani wafanyakazi na wananchi kwa ujumla wanapata taabu ya nyumba za kuishi, hata ofisi kwa taasisi mbalimbali za Serikali na Mashirika ya watu binafsi. Ninaomba Mkurugenzi huyu awasiliane na Mkuu wa Mkoa wa Singida ili kupata maelezo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo inawasaidia wajasiliamali katika kujifunza zaidi na kupata nafasi kuuza bidhaa zao kupitia maonyesho mbalimbali yanayofanyika kitaifa na kimataifa. Ninaishauri Serikali kushirikisha wafanyabiashara mbalimbali hasa wajasirihamali ili kujifunza zaidi na kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida una wajasiliamali wengi sana, lakini wanaopata mialiko kwenda kwenye maonyesho haya ni wachache sana. Ninaomba Serikali kupanua wigo huu ili wajasiliamali wengi wapate nafasi hii adimu. Vile vile kuwapunguzia gharama kwa kuwapa mabanda kwa bei nafuu na bure ikiwezekana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono bajeti hii mia kwa mia wakati nikisubiri ufanuzi wa Mheshimiwa Waziri wakati wa majumuisho yake.

**MHE. MGANA I. SINDAI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara yake na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, napenda nifahamu mikopo ya vijana iliyokuwa inapitia Halmashauri za Wilaya imefikia wapi. Maana inaonyesha sasa hivi haipatikani, mikopo iliyokuwa inawasaidia sana vijana kujiondolea umaskini kwa kuanzisha miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, napenda nijulishwe, zile ajira 1,000,000 zilzitotamkwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete zimefikia wapi? Sasa tupo nusu ya kipindi cha miaka mitano. Je, Mpaka 2010 nafasi hizo zitakuwa zimefikiwa?

Mheshimiwa Spika, mamilioni yaliyotolewa na Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete inaonyesha hayakuwafikia walengwa. Je, Wizara yako imechukua hatua gani kurekebisha mapungufu hayo?

Mheshimiwa Spika, *SACCOS* ndio njia pekee ya kuwawezesha wananchi wote wapate mikopo kwa ajili ya kujileta maendeleo. Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha *SACCOS* zinaendelezwa kwenye vijiji/Kata zote hapa nchini?

**MHE. AZIZA SLEYUM ALLY:** Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya na ushirikiano wake na kujitolea kwa jamii nzima. Pia na wapongeza watendaji katika Wizara pamoja na Mashirika na Taasisi zote.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aende Tabora kufanya ziara katika Kiwanda cha Nyuki na kuzungumza na wafanyakazi wote. Haya ni maombi ya wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Spika, napata wasiwasi kuhusu ajira za vijana na kwa kuwa vijana hawa wana wazazi wao: Je, Serikali haionti kwamba kuna haja ya kujenga uwezo wa vijana katika kushiriki kuwapa elimu ya utengenezaji vifaa vidogo vidogo kwa kushirikiana na *SIDO*? Nadhani vijana wengi wawe na ujuzi wa kuwandoa na ujinga wa kutopata ujuzi wowote.

Mheshimiwa Spika, naomba, niipongeze taasisi ya *NSSF* pamoja na *PPF* kwa kazi wanazofanya za kuonekana na zile za kiofisi ambazo hazionekani. Pia napenda kuipongeza *NSSF* na Mkurugenzi wao Ndugu Dau Ramadhani kwa kufanya kazi nzuri sana katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Hakika Watanzania wanaweza wanapoamua. Nawapongeza kwa kujenga majengo mazuri katika chuo hicho na kwa muda mchache sana eneo la msitu limebadilika na kuwa mahali pazuri sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARGARET AGNES MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mheshimiwa Prof. Kapuya, Naibu Waziri - Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa hotuba nzuri yenye kina inayoleweka vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kusikia kuwa Serikali na sekta mbalimbali zinaweza kukuza ajira na kwamba lengo la ajira milioni moja litafikiwa. Hata hivyo, naomba ufanuzi kuwa mkakati gani mahsus umeandaliwa na Wizara kuhakikisha

vijana wenyе ulemavu wanapata ajira rasmi na ya kujiajiri hasa ikizingatiwa kuwa waajiri binafsi walio wengi wanawaona watu wenyе ulemavu hawawezi kutoa tija? Nashauri Chama cha Waajiri nacho kitoe mwongozo. Zaidi ya hayo naomba Serikali ione uwezekano wa kutoa motisha kwa waajiri binafsi wanaojiri wenyе ulemavu nchini.

Naipongeza Kampuni ya kutengeneza vifaa vya ngozi ya Sheah huko Arusha ambayo imeajiri watu wenyе ulemavu wengi ingawa kampuni haina motisha yoyote. Nitahitaji kupata ufanuzi katika ajira za sasa, ni vijana wenyе ulemavu wangapi wamefaidika?

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la mikopo ya mfuko wa vijana. Katika hili ni walemvu wachache sana nchini wamefaidika na mkopo huu. Hii ni kwa vile wengi wao hawana elimu, wala uandikaji wa michanganuo ya miradi. Nahitaji Wizara iwe na mkakati maalum wa kuiwezesha jamii ya vijana walemvu kupata mafunzo ya ujasiriamali na ushirika wa *SACCOS* ili waweze kujiajiri kwa mtaji wa mikopo husika. Kinyume cha hayo vijana hawa wataendelea kuwa omboomba kama inavyojitokeza kwenye miji mingi hapa nchini, tunawaona Dar (barabarani) na kadhalika. Iteleweke kuwa wao ndio fukara/masikini zaidi kuliko wasio walemvu.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huu, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri - Prof. Kapuya, Naibu wake - D. M. Mahanga, Katibu Mkuu - Dr. L. Komba akiwemo Msaidizi wake Bi. E. Mangesho ambao kwa pamoja wameleta hoja nzuri ambayo imegusa maeneo mengi yanayohusu Wizara nzima. Naunga mkono hoja hii kwa hali zote.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo ambayo bado ninaiomba Wizara ione namna ya kufuatilia ushauri na maombi yangu kwa Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na *NSSF* kufanya kazi nzuri katika nyanja nyingi zikiwemo za ujenzi wa Majengo mbalimbali, bado napenda kukumbusha ombi langu la mwaka jana kuwa Rais aliagiza Wizara, Mashirika na Taasisi mbalimbali yaone namna ya kusaidia Mikoa ya pembezoni kama Rukwa, Tabora, Kigoma, Singida.

Kwa Mkoa wa Rukwa ambao hivi karibuni barabara ya lami itanza, *NSSF* tuiombe ianze mipango ya kujenga nyumba za ofisi za kupangisha na nyumba za kukodi Mjini Sumbawanga. Niko tayari kuwatafutia *prime areas* kwa madhumuni hayo.

Mheshimiwa Spika, bado Wizara inawajibika kukamilisha uundaji wa Baraza la Vijana ili vijana wawe na mahali pa kuzungumzia mustakabali wa maendeleo yao kwa kuna na ushauri kwa Wizara juu ya njia nzuri za kuwatumia vijana katika shughuli za kuongeza ajira. Nashauri vijana waanze kuandaliwa kujiunga na shughuli za kilimo. Maeneo mengi yaliyotengwa mwaka 1999 huko Kisarawe kwa shughuli hizo za kilimo yatizamwe upya.

Mheshimiwa Spika, nini azma ya kuendelea na sera ya mapato, tija na bei katika mazingira ya hivi sasa? Sera hii iangaliwe na hali ya ajira na mishahara ambayo kila kukicha, tofauti kati ya mishahara ya kima cha chini na cha juu inazidi kupanuka sana. Hali hii siyo nzuri kwa usalama wa Taifa. Hapa ni vizuri vikao vya *Utatu* vikapewa umuhimu wa pekee ili kutumia uzoefu wa pande zote katika kujenga mazingira yasiyo na utata kwa upande zote husika.

Mheshimiwa Spika, hali ya vijana wetu bado ni tete. Wengi bado wanadhani Serikali inawafanya kila kitu. Nashauri, kwa kutumia *ILO* Wizara iandae mpango kambambe ambao utasaidia kufikia lengo la Ilani la kufikia ajira mpya milioni moja na kuendelea. Serikali za Mitaa nazo zisidhani jukumu hili ni la Wizara pekee yake. Huko Wilayani ziko shughuli nyingi ambazo zinafanywa kama za uvuvi, kilimo, ufugaji wa mifugo na urinaji wa asali; uchimbaji wa madini na kadhalika. Inaonyesha kuwa yote hayo hayajumuishwi kwenye ajira mpya za vijana wetu, sijui kama tukishashughulikia kwa kutazama suala tu la wamachinga tutaweza kulitatu tatizo hili!

Mheshimiwa Spika, mengine naungana na ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama (Mb) kuhusu umuhimu wa kuvijenga na kuvisimamia vizuri vyama vya wafanyakazi ili visaidie kujenga umoja, uelewa na kuimarisha mashauriano ya pamoja katika kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BUJIKU PHILIP SAKILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa kwa hotuba yake nzuri sana. Ninaamini kukaa kwake katika Wizara hii kwa kipindi cha pili sasa, bila shaka kumemsadia kuyafahamu fika matatizo yaliyomo katika Wizara hiyo. Aidha, kumemwezesha kufahamu njia muafaka ya kutatua matatizo ya kiutendaji kila yajitokezayo Wizarani kwa kuwa karibu na vyama uhuru vya wafanyakazi navyo vimechangia sana katika utendaji Wizarani humo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la *NSSF* limeonyesha umahiri mkubwa sana katika miradi yake mbalimbali hususan inayolenga kumwondolea kero mbalimbali mwanachama wake. Aidha, nalipongeza kwa kujiwekea umuhimu wa kuchangia katika miradi inayoibuliwa na kutekelezwa kwa nguvu za wananchi. Mfano mzuri ni kwa jimbo la Kwimba, ni msaada wake kwa ujenzi wa Maktaba katika Shule ya Sekondari Mwanshimba iliyo na kidato cha tano na sita kwa wasichana. Kwa niaba ya jumuia nzima ya shule hii, ninaomba uongozi wa *NSSF* ukubali kupokea shukrani zao za dhati kupitia mimi Mbunge wao.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili la *NSSF* limekuwa likishiriki katika miradi mbalimbali. Moja ya miradi iliyonivutia sana ni ujenzi wa nyumba zenye gharama nafuu. Katika Makao Makuu ya Wilaya ya Kwimba ambayo iko katika Mji wa Ngudu, makazi ni ya shida sana. Mji huu unakua haraka, hivyo watumishi wakiwemo wanachama wa *NSSF* wanapata shida sana kupata mahali/nyumba za kupanga.

Nimekuwa nikifuatilia sana kuona kama *NSSF* inaweza kupata fursa ya kujenga nyumba 30 – 50 katika Mji wa Ngudu, nyumba zitakazokuwa zinafanana kwa gharama na muundo wa nyumba zilizijengwa na *NSSF* Kinyerezi jijini Dar es Salaam. Ni muafaka sasa kujenga nyumba kama hizo kwa kuwa bado kungali na maeneo ya wazi mengi. Naomba nitumie fursa hii tena kuiomba *NSSF* kwa mara nyingine kulikubali ombi langu la kuja kufunga mkataba na Halmashauri ya Kwimba, mkataba utakaoliwezesha shirika hili kuanza kujenga nyumba Kwimba.

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni Serikali kujenga mazingira mapema ya kuwezesha Shirika la *NSSF* kuanza kujenga daraja la Kigamboni sasa. Kadri tunavyozidi kuchelewa gharama ya ujenzi ndivyo itakavyokuwa ikizidi kupanda na kuongeza uzito wa mzigo huu kubebwa na *NSSF* na Taifa kuubeba. Kadiri uzito wa mzigo huu utakavyokuwa umeongezeka, ndivyo uzito wa mvuto wa kuahirisha au kuacha kabisa ujenzi huo utakavyokuwa unaongezeka. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kukutanisha pande zote zinazohusika kufunga mianya yote inayozuia ujenzi wa daraja hilo mapema.

- Mheshimiwa Spika, baadhi ya faida za daraja hilo ni pamoja na:-
- (1) Kupanua jiji la Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kuongeza makazi;
  - (2) Kupunguza msongamano ya magari katikati ya jiji;
  - (3) Kupendezesha jiji;
  - (4) Kufanya mawasiliano kuwa rahisi kwa kwenda na kurudi Kigamboni bila shida kubwa; na
  - (5) Itaongeza wigo wa mapato ya jiji na Taifa.

Mheshimiwa Spika, faida hizi na nyingine nyingi tunazikosa kwa kutokukamilisha ujenzi wa daraja hili.

Mheshimiwa Spika, uwezo wa *NSSF* unajionyesha dhahiri katika ushiriki wake katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Uwezo huu unatisha na ninawapongeza kwa dhati.

Mheshimiwa Spika, mgogoro wa Kiwanja cha Shirika la Taifa kilichochukuliwa na *IMTU*, kinachotokea hakieleweki vizuri. Kilichotokea ni sawa na mtu kumtoa mtoto wake wa miaka mitano kutoka kwenye kitanda chake kilicho na chandaria na kumlaza chini bila godoro wala chandaria na kumwachia mtoto mgeni kwa kisingizio cha kutokuwa na ubaguzi na upendo. Kama hana ubaguzi, kwa nini asiwafanye wote walale kwenye kitanda kimoja au yeye mwenyewe kumwachia mtoto mgeni kitanda chake?

Mheshimiwa Spika, kilichotokea kinashangaza sana. Inaelekea uamuzi huo ulifikiwa bila kutathmini umuhimu wa shughuli za Shirika la Tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mipango ya mbele ya shirika hili, laiti kama umakini ungekuwa umechukuliwa kabla sana ya kufikia uamuzi wa kulinyang'anya shirika hili na shughuli zinalozifanya, uamuzi huu ninaamini ungefikiriwa. Kipimo kidogo tu cha

kizalendo kingetosha kusema uamuzi huo haukuwa sawa. Ombi langu ni kuishauri Serikali ipitie tena uamuzi huu na ichukue moja kati ya ushauri huu.

- (1) Shirika la *TIJA* lirezeshewe kiwanja chake bila malipo yoyote zaidi ya kiasi lilolipwa na *IMTU*;
- (2) Lipewe kiwanja kingine kama hicho bure; na
- (3) Lirezeshewe gharama zake zote lilizotumia kwa kugharama ya sasa

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na Kifungu 16(h) Uk.14 na kiambatanisho No.III naelewa kuwa ukopaji usioridhisha na wajasiriamali wa wilaya ya Ludewa inatokana na kutokuwepo kwa *SACCOS* na uelewa mdogo kuhusu mpango huu kama hotuba ilivyoainisha katika kiambatisho Na. J uk.72 .

Je, Wizara itatusaidia vipia kuondokana na changamoto hizi? Kwa nini *SACCOS* mpya ya Mlangali *SACCOS* wilayani humo haijakopeshwa?

(1) Kwa vile tayari kuna vikundi vya vijana vinavyojishughulisha na utengenezaji maboti ya kisasa na uvuvi endelevu katika mwambao wa Ziwa Nyasa Wilayani Ludewa: Je, Wizara itawasaidiaji wanavikundi hawa kupata mikopo kwa ajili ya kununulia vifaa vya ujenzi wa maboti na zana za uvuvi endelevu?

(2) Kutokana na kuwepo vikundi kadhaa katika mwambao wa ziwa Nyasa Wilayani Ludewa vinavyojihusisha na ufinyanzi vyungu vya mapambo na matumizi ya nyumbani kutokana na kuwepo na raslimali (udongo) ya kufinyanga vyungu iliyopo kwa wingi sana na teknolojia hiyo ya asili: Je, Wizara inaahidi kuwasaidiajie wanavikundi hawa kuboresha teknolojia ya ufinyanzi na kupata masoko hapa nchini na nje ili wajikwamue na umaskini?

**MHE. DR. WILBROD PETER SLAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna malalamiko mengi ya unyanyasaji wa wafanyakazi kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu kutoka kwa waajiri katika sekta mbali mbali binafsi na kwa vile waajiri wengine wanawakataza kabisa wafanyakazi wao kuijunga na vyama vya wafanyakazi kwa kuwalazimisha kuweka saini mkataba ili ionekane wafanyakazi wameamua kwa hiari yao:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa umma mkubwa wa wafanyakazi Watanzania ambao ndani ya nchi yao wameonyesha kukata tamaa kwa vile hawana mtetezi na vyama vyao vimeonyesha udhaifu mkubwa katika kusimamia maslahi ya wanachama wao?

(b) Kwa vile Serikali imetoa kima cha chini cha mishahara ya watumishi wa umma/Serikali: Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kulieleza Bunge hili, kima cha chini katika sekta binafsi ni kiasi gani? Je, Serikali ina mfumo gani au chombo gani kuhakikisha na kusimamia waajiri binafsi wanalipa kima hicho cha chini bila bughudha na usumbufu wowote kwa wafanyakazi?

(c) Pale ambapo vyama vya wafanyakazi vinaonekana dhaifu na au vinakula njama na waajiri na kuonekana kusimama upande wa waajiri serikali inatoa kauli gani?

Mheshimiwa Spika, kwa vile kuna wafanyakazi wengi ambaa baada ya ubinafsishaji wamepoteza ajira zao na hawakulipwa haki zao kama ilivyotokea kwa wafanyakazi na *SPM – Mgololo, AMI – Kigoma* – waliokuwa watumishi wa *TPA* na suala lao nilikwishalifikisha kwa Mheshimiwa Waziri, Serikali inachukua hatua gani ili watumishi hawa, Watanzania ambaa wameathirika na mabadiliko ya sera na hivyo wao na familia zao kuathirika kiuchumi, kijamii na kisaikolojia?

Mheshimiwa Spika, Serikali inaweza kulieleza nini Bunge hili kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kutengeneza ajira millioni moja katika kipindi cha miaka mitano? Kwa vile punde tutakuwa tumekamilisha miaka mitatu tangu Uchaguzi Mkuu ambapo ahadi hiyo ilitolewa: Je, ni ajira ngapi mpya zimetengenezwa kwa maamuzi ya makusudi ya kutekeleza ahadi hiyo? Ajira hizo ziko kwenye sekta zifi za umma na binafsi na mchanganuo wake wa kina?

Mheshimiwa Spika, Bunge hili Tukufu lilipitisha Kituo cha Taifa cha Ajira kwa sheria rasmi ya Bunge; na kwa mujibu wa sheria hiyo vituo hivyo vinatakiwa kuundwa hadi kwenye ngazi ya Wilaya. Ni muda mrefu sasa tangu sheria hiyo ilipopitishwa. Waziri anaweza kulieleza Bunge hili ni nini mafanikio ya kituo hicho katika ngazi ya Taifa, yaani ni Watanzania wangapi wamepata ajira zao kupitia kituo hicho? Kama hakuna mafanikio, ni kwa nini? Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na vituo hivyo katika ngazi ya Wilaya kushindwa kabisa kuanza kazi?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nitangulie kwa kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Makamu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba tunayojadili.

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Uchaguzi Mkuu, mwaka 2005, ukurasa 126, Ibara ya 103, Vifungu vidogo (a), (b), (c) na (d) vinatamka wazi ni jinsi gani vijana wetu watasaidiwa na Serikali endapo CCM itaingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, Mungu akabariki, CCM ikaingia madarakani kwa ushindi mkubwa. Ni miaka mitatu sasa, tangu Serikali ya awamu ya nne iingie madarakani, lakini baadhi ya mambo yaliyoainishwa kwenye ilani yanakwenda kinyume cha matarajio ya wananchi hususani ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, agenda ya ajira ni jambo kubwa duniani na linasumbua hata nchi zilizoendelea. Uchumi wa nchi unapokuwa duni, changamoto inakuwa kubwa sana. Mbaya zaidi, ongezeko la uhalifu sehemu nyingi duniani linachangiwa pia na ukosefu wa ajira.

Mheshimiwa Spika, takwimu za vijana wasio na ajira, sasa hapa kwetu hebu tuijulize hivi, tunazo takwimu sahihi za vijana wasio na ajira? Wangapi wana ujuzi? Wangapi hawana ujuzi? Wangapi tatizo ni mtaji? Kwa sababu wanazo shughuli za uzalishaji walizo na uzoefu nazo bali wanakwama. Ajira za msingi kwetu ni zile za uzalishaji kuliko za huduma, kwani hizi zinakuza uchumi wetu. Baada ya kupata takwimu sahihi, tuangalie kama sekta zote hasa za uchumi zinalenga kuongeza ajira. Kilimo kimeongeza ajira ngapi mwaka jana na mwaka huu kitaongeza ajira ngapi? Viwanda vitaongeza ajira ngapi? Madini nayo itaongeza ajira ngapi? Na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha atupatie takwimu kwa kila Wilaya na kila Mkoa ajira ngapi ziliongezeka mwaka jana na mwaka huu ni ngapi zimewekwa kuwa lengo.

Mheshimiwa Spika, ninachosisitiza hapa, ni kwamba kila sekta lazima iwe na malengo ya kuongeza ajira na hivyo hivyo kwa kila Wilaya .

Mheshimiwa Spika, baada ya kuweka malengo, mipango ibuniwe. Tukumbuke kuwa, juhudhi bila mwelekeo na malengo sio kipimo cha maendeleo, tufanye tathmini kila mwaka kujua nani amezalisha ajira na ni ngapi. Nashauri kipimo cha utendaji kazi serikalini, kiwe ni ajira ngapi wilaya imezalisha.

Mheshimiwa Spika, hapa ninashauri tufanye kama tulivyofanya katika kupanua nafasi za sekondari za Kata kwa watoto wetu wanaofaulu darasa la saba. Pamoja na changamoto zilizojitokeza kwa kuanzisha shule mpya nyingi nchini kote, hili ni jambo la kujivunia kwa sababu tunasonga mbele. Tuwe na takwimu sahihi za vijana wasio na ajira kwa kila Wilaya na zionyeshe umri, elimu na mafunzo na uwezo wa kila kijana. Kisha tuweke lengo kwa kila Wilaya ya kubuni mipango na kuwezesha asilimia fulani ya vijana kupata ajira. Juhudi za kuongeza ajira zionekana wazi wazi kwa kila Wilaya, kila kiongozi, kila mtendaji akose usingizi kwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, tusipowaonyesha vijana wetu juhudhi zetu za kuwawezesha kupata ajira, hawataturelewa na matokeo yake ni mabaya, sio kisiasa tu, bali hata kiusalamu.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua fursa tulizonazo zinatokana na maliasili zetu. Ardhi nzuri ya kilimo, mazao ya misitu, mazao ya mifugo na kadhalika. Tunatakiwa kuwapa vijana ujuzi na vitende kazi vya kuzalisha katika sekta hizi tulenge kila kijana mwenye afya awe na ajira kwa ajili ya mahitaji yake na kuchangia kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana na ninaamini hoja/maswali yangu yatajibiwa vyema.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja. Nitachangia eneo moja tu ambalo naiomba Wizara ilifikirie kwa kina, nalo ni Mpango wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi na kukuza ajira.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa mikopo ya wajasiriamali kupitia Benki za *CRDB* na *NMB*. Fedha nyingi imetoka na wananchi wengi wamefaidika.

Wakati utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi (kupitia benki na asasi ndogo ndogo za fedha) unaanza, Serikali izingatie kuwa wakulima wengi hawakufaidika na mpango huu. Kwa upande wa wakulima wa Kyela, kikwazo kikubwa ni masharti ya kukopa fedha hiyo. Nitatoa mfano:-

Mkulima wa mpunga anahitaji miezi tisa toka awekeze fedha aliyokopa hadi kuvuna mpunga. Mkulima wa ndizi miezi 12, mkulima wa korosho miezi tisa na mkulima wa kokoa ni miezi saba. Masharti ya ukopeshaji fedha hiyo ya uwezeshaji yazingatie kipindi hicho cha uzalishaji kwa upande wa mkulima. Bila kufanya hivyo, mikopo hii itaendelea kuwa ya wafanyabiashara wadogo wadogo wa mijini. Naiomba Wizara ilitupie suala hili jicho. Hoja ya kwamba *SACCOS* zitafanya kazi hiyo haisaidii kuilewa hali hii ya wakulima ambao bado wanachangia sehemu kubwa ya pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema, naunga mkono hoja.

**MHE. JACOB DALALI SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Niungane na wenzangu kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na Wakurugenzi wote wanaowasaidia.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ambayo kama itatengewa pesa nzuri kulingana na mipango yao, itatufanya tuzalishe zaidi kwa sababu kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi atafanya kazi ambayo itampatia kipato na ziada itapatikana. Hivyo, kuna umuhimu wa Wizara hii kuungwa mkono kwa mipango yake. Kila aliye na uwezo wa kufanya kazi afanye kazi kwa faida yake na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi inavyo vikundi vingi, baadhi havijasajiriwa. Mikakati ya kuwaandaa tayari, tumefanya vikundi vinane vimepatiwa pesa na viko karibu kumaliza mikopo yao.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi na Sengerema na Shirika la *SLEM*. Vikundi mbalimbali vimekuwa na jukwaa la wadau wao wenyewe wanacho chombo cha kuratibu mikopo yao. Chombo hicho kina jina la MKUKUWAMI. Jina hilo limebuniwa kwa nia ya kuwaunganisha wadau. Jukwaa hilo la wadau wamenitura niiombe Serikali ipitishe pesa zote za wajasiliamali kwa mfano pesa za *SLEM* zinategemea kupitia huko

shilingi milioni 200 zinategemewa na wananchi hao. Tunaomba sana pesa za JK zipitie huko.

Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani kwa jinsi Serikali ilivyoliona tatizo la kutupatia pesa za JK awamu ya kwanza. Hata hivyo, Wizara hii ililliona tatizo hilo na kulitatua kwa kutumia chombo cha wanaushirika *SCCULT*. Chombo hiki kimegawanya vizuri, pesa zilizotolewa safari hii Wilaya ya Misungwi uongozi wa Wilaya umeshiriki kugawa kiasi cha shilingi milioni 50, Juni na Julai waliopata ni kama ilivyoonyeshwa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Sungusungu Shilalo Sh. 5,000,000/=, Jitegemee Sh. 5,000,000/=, Misasi *SACCOS* Sh.10,000,000/=, Wabuki – Sh.5,000,000/= na Kakolo Bukumbi Sh.5,000,000/. wajasiliamali hawa wanaipongeza Serikali na wanaomba tu *SCCULT* wapunguze taratibu zao kwa mfano ukikopa Sh. 200,000/= inawapasa muwe na theluthi moja katika akaunti yenu. Hili ni tatizo ambalo vikundi hivi ndiyo vinaanza kujipanga. Naomba mkopo utolewe bila masharti.

Mheshimiwa Spika, wapo wafanyakazi wanapopata uhamisho kwenda kufanya kazi sehemu nyingine, tatizo ni malipo ya uhamisho. Ni tatizo! Familia zao huziacha mbali na hasa watumishi wa Halmashauri, hivyo Wizara hii kwa maana ya Serikali Kuu saidieni sana tatizo hilo kwa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *NSSF* kwa kazi nzuri ya ujenzi wa vitega uchumi hapa nchini. Mimi kama Mbunge wa Misungwi Mkoani Mwanza tumeona kazi iliyofanyika **KISEKE!** Ni nyumba nzuri na zitapunguza matatizo ya wanachama na wananchi. Lipo jengo kubwa eneo la *Kenyatta Road*, ujenzi huu/uwekezaji huu mimi kwa niaba ya wananchi wa Mwanza tunaomba sana mpokee shukrani kwa kazi nzuri, endeleeni kujenga na kuuza ili akiba ya wafanyakazi isiyumbishwe na vitega uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomb sana Wizara ijenje nyumba za kuuza eneo la Misungwi kwani ni Kilometra 30 tu toka Mwanza mjini. Hadi sasa wapo watumishi wamejenga nyumba zao na wanafanya kazi jijini Mwanza.

Mheshimiwa Spika, shukrani za mwisho ni kwa Katibu Mkuu - Dr. Komba kwa kazi nzuri. Aendelee kutetea wafanyakazi wote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawapongeza Waziri - Mheshimiwa Alhaj Juma Kapuya na Naibu Waziri – Mheshimiwa Makongoro Mahanga, Katibu Mkuu na watendaji wote. Nawapongeza kwa hotuba nzuri yenye kutia moyo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitajikita kwenye upande wa ajira. Vijana wengi ni wazururaji na wana hali ngumu sana kimaisha. Je, Serikali inawafikiriaje vijana hawa? Wizara ingegawanya hizo ajira ilizoahidi kwenye Wilaya zote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya mwaka 2005 inaelekeza kuwa sehemu kubwa ya jamii ya Watanzania ni vijana. Elimu ya kujitegemea, Elimu ya Ufundu na stadi nyingine inasisitizwa ili waweze kujajiri.

Mheshimiwa Spika, katika suala la kuwahamasisha vijana ili waweze kujiunga katika vikundi mbali mbali vya ushirika ukiwemo ushirika wa kuweka na kukopa (*SACCOS*): Je, vijana hao pamoja na kujiunga, pamoja na kuanzisha vikundi hivyo, wamewezeshwa na hiyo mikopo? Tunaiomba Serikali iweke mikakati ili fedha hizo ziwafikie walengwa.

Mheshimiwa Spika, lingine, ni kuhusu ajira kwa watu wenye ulemavu. Kundi hili maalum kwa upande wa ajira ni matatizo makubwa. Mtu mwenye ulimavu anaweza akawa na ujuzi na sifa zote kwa ajira iliyotangazwa, lakini ikifika wakati wa mahojiano, hapo ndiyo penye tatizo. Atahojiwa na atafanya vizuri, lakini hapewi ajira, kisa ni mlemavu. Kwa kweli hii siyo haki. Naomba Mheshimiwa Waziri alone hilo, alitetee kwani nao wana haki ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nalipongeza Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*) kwa kuwekeza kwenye vitega uchumi mbalimbali kama dhamana za Serikali, mikopo, hisa za makampuni yaliyosajiliwa katika soko la hisa la Dar es Salaam na makampuni yasiyosajiliwa na katika ujenzi wa nyumba na ofisi za kupangisha au kuuza.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii ili niseme/nichangie machache kuhusu bajeti ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka huu wa fedha 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, Shamba la Sasanda – Mbozi – Mbeya lenye ukubwa wa zaidi ya ekari 800 lipo Wilayani Mbozi na liko chini ya Wizara hii. Shamba hilo, kwa taarifa ya Wizara limetengwa kama Kambi ya Vijana kwa maana ya kutumika kwa shughuli za vijana. Hata hivyo, shamba hili kwa miaka mingi limekuwa halitumiki sawa sawa. Matumizi yake ni kidogo sana, chini ya asilimia 30 ya eneo lote.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007/2008 wakati Wizara hii inapitisha bajeti yake hapa Bungeni niliwahi kusema kwamba mahitaji ya ardhi kwa wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususani Mbozi Mashariki, ni makubwa sana. Niliwahi kuomba kwamba tupewe sehemu ya ardhi hiyo ili tujenge shule (hata ekari 50) lakini Wizara ilikataa. Sababu zilizotolewa na Wizara ni kwamba, imejizatiti kikamilifu kuliendeleza eneo hilo na kulitengwa kiasi cha kama milioni 50 hivi (2007/2008).

Mheshimiwa Spika, Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie, kiasi hicho cha shilingi milioni 50, kimefanya kazi gani? Aidha, nataka kujua: Je, mwaka huu 2008/2009 ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kuendeleza eneo hilo? Je, kama kuna

kusuasua namna hiyo, sio vizuri sasa Wizara ikatoa eneo angalau la ekari 50 hadi 100 kwa ajili ya shughuli nyingine za maendeleo?

Naomba majibu ya kuridhisha, vinginevyo sitaunga mkono bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nimesoma vizuri hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuhusu namna *Labour Exchange Centre* inavyofanya kazi. Ukisoma haraka haraka, utaona kwamba kituo kimefanya kazi nzuri. Hata hivyo, ambacho sina hakika nacho ni namna kituo kinavyohusika kuwatafutia vijana na Watanzania wengine kazi badala ya kuwaunganisha na waajiri tu bila kujua kama wamefanikiwa kupata kazi au la. Nashauri kituo kiende hatua kubwa zaidi kuliko sasa. Aidha, nashauri kituo chenyewe kiboreshwe, maana jinsi kilivyo leo hakitoi picha nzuri sana. Kiboreshwe kuanzia jengo, samani (*furniture*) vifaa vya kazi kama vile kompyuta na kadhalika. Ni vizuri pia maslahi ya wafanyakazi yaboreshwe. Nachelea kusema kwamba huwezi kuwa na moyo wa kumtafutia mtu mwingine kazi wakati wewe mwenyewe una kazi ya hovyo hovyo, yaani maslahi duni na mazingira mabaya ya kazi.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mikopo, maarufu kama “mikopo ya JK” imekwisha na sasa tunakwenda kwanza awamu ya pili. Ni kweli kwamba awamu ya kwanza ya mikopo ilifaidisha zaidi watu wa mijini kuliko wa vijiji kwa kuwa tayari zimeteuliwa taasisi 14 za kifedha kwa ajili ya kupeleka mikopo vijiji. Naomba Mheshimiwa Waziri na Wizara hii isimamie vizuri zaidi awamu hii ya pili ya mikopo ili iende vizuri zaidi kuliko ilivyokuwa awamu ya kwanza.

Aidha, Wizara idhibiti vitendo vya rushwa ambavyo vinasabishwa na Maafisa Mikopo na Taasisi husika. Nasema hivyo kwa sababu awamu ya kwanza mikopo iliandamana na shutuma kutoka kwa wakopaji kwamba Maafisa Mikopo wa Benki walikuwa wanahonga asilimia kumi ya mikopo wakidai kwamba wanafanya kazi ngumu sana. Naomba sana hili lisijirudie katika awamu hii ya pili ya mikopo hiyo.

Ahsante sana.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, napenda awali ya yote nitoe rambirambi kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi, hususan wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi kwa Mheshimiwa Severina Mwijage kutokana na kifo cha mtoto wake na dereva kutokana na ajali ya gari lao iliyotokea asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa hotuba yake ya bajeti yenye kuleta matumaini makubwa kwa wananchi wa Taifa hili, hususan vijana wetu. Napenda pia nitoe pongezi nyingi kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Watendaji na Wakuu wa Mifuko ya Pensheni na Taasisi zilizoko chini ya usimamizi wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na pia kwa kushiriki kikamilifu katika kutayarisha hotuba ya Mheshimiwa Waziri yenye kila sifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda nijikite katika maeneo yafuatayo:-

- (1) Mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI/UKIMWI mahali pa kazi;
- (2) Ajira kwa vijana;
- (3) Mikopo ya mabilioni ya Kikwete wilayani na vijijini;
- (4) Usalama na afya mahali pa kazi; na
- (5) Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*).

Mheshimiwa Spika, napenda niimpungeze Wizara hii kwa mipango, mikakati yake kuhusiana na mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI na UKIMWI mahali pa kazi, ambapo ndipo walipo vijana wenyewe jukumu la kusukuma mbele gurudumu la maendeleo ya Taifa katika nyanja zote, hususan kuinua uchumi wetu. Ni imani yangu Wizara imechelewa ama imechukua muda mrefu mno kukamilisha uchapishaji na kutafsiri kwa lugha ya Kiswahili kitabu cha “HIV/AIDS Code of Conduct”, ambacho ni mwongozo wa msingi wa mapambano dhidi ya janga hili katika makundi mbali mbali ya wafanyakazi.

Naishauri Wizara ikamilishe mchakato huu haraka iwezekanavyo ili kuwapa fursa wafanyakazi ya kushiriki kikamilifu katika vita dhidi ya Ukimwi.

Nashauri pia Serikali iongeze fungu la fedha kwa Wizara hii ili iweze kutekeleza jukumu la kufikisha kitabu hiki kwa wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, vijana wasiokuwa na ajira ni bomu linalosubiri kulipuka, idadi kubwa ya vijana wetu wanamaliza shule na vyuo na kasha kukimbilia mijini kwa matumaini ya kupata kazi za kuajiriwa maofisini. Wizara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha vijana hawa wakiwa bado shulenii na vyuoni wahamasishwe kuwa tayari kufanya kazi za kujajiri.

Wizara ya Kazi, kuititia wataalam wake Mikoani, ihakikishe vijana wanafikishiwa elimu sahihi ya ujasiriamali kwa muda muafaka na hivyo kuwawezesha kuthamini stadi mbalimbali za maisha. Mlundikano wa vijana sehemu za Mijini ndiyo kitovu cha maovu mbalimbali ikiwa pamoja na ujambazi, utumiaji wa dawa za kulevyta, uzinzi na ubakaji. Wapewe nyenzo za maisha na kupewa nafasi za kujiendeleza kiuchumi kwa kupewa mitaji mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mikopo ya mabilioni ya Kikwete, pamoja na lengo na nia njema ya kuanzisha, lakini utawanyaji wake hususan awamu ya kwanza umekuwa mbaya sana ambaao haujasaidia walengwa katika maeneo mengi ya nchi hii hususan yale ya vijijini kama yale ya Jimbo la Mbozi Magharibi. Awamu ya kwanza ya mgao ilijaa usumbu mkubwa kwa wananchi kiasi cha kufikia hatua ya unyanyaswaji kwao na hata kukashifiwa na/ama Maafisa Ushirika kwenye Halmashauri, ama Uongozi wa Benki zilizopewa dhamana ya kutekeleza jukumu hili.

Jimbo la Mbozi Magharibi, kutokana na kuwa pembezoni na Benki za *CRDB* na *NMB* halijanufaika hata kidogo na mikopo hiyo. Naomba Serikali itafute namna nzuri ya kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, suala la usalama na afya mahali pa kazi ni la umuhimu wa pekee ili kuhakikisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa wafanyakazi bila kujali mahali hapo ni eneo la ajira binafsi, ya shirika au ya umma. Matukio mengi ya ajali mbaya au milipuko ya magonjwa ambayo husababisha vifo au vilema ni matokeo ya ukosefu wa utekelezaji wa sheria, taratibu na kanuni za usalama na afya mahali pa kazi.

Ni wakati muafaka kwa Serikali kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya ukiukwaji wa sheria na kanuni hizi. Mifano, ujazaji wa abiria kupita kiasi kwenye mabasi na malori, uendeshaji wa vyombo vya moto vibovu, umwagaji uchafu/takataka ovyo sehemu zisizostahili kwenye maeneo yanayotuzunguka, barabarani, sokoni na majumbani. Naamini sheria zipo, ukaguzi ufanywe na wahusika wawajibishwe kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda niivilie kofia *NSSF* kwa kazi nzuri ambayo shirika hili la Hifadhai ya Jamii linafanya. Matokeo ya ufanisi wake yanaonekana katika maeneo mbali mbali ya nchi hii na hata nje ya nchi. Shirika hili linastahili medali ya utendaji uliotukuka. Ufadhilli wa ujenzi wa nyumba mbalimbali za kuishi, ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Dodoma ya kuwezesha wanafunzi 20,000 na ushiriki wake katika mpango wa kujenga daraja la kigamboni ni mfano halisi ya uzalendo wa uhakika wa uongozi wa *NSSF*.

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja .

**MHE. JUMA KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Alhaj Prof. Juma Athuman Kapuya (Mb) na Naibu wake - Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga (Mb). Pia nawapongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana hasa kwa sekta ya vijana kwa malengo, rika lote la vijana ni lazima majukumu ya maendeleo yake yapo mikononi mwa Wizara hii. Zipo sababu ambazo zinachangiwa kwa makusudi na Watendaji wa Wizara hii katika kukumbusha maendeleo ya vijana.

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu zifuatazo:-

Kutokana na mfumo *horse* ni dhahiri Wizara yenyewe watendaji wake wameachwa na umri katika maana hiyo kwa makusudi hawatapenda sana kutekeleza majukumu ya vijana kimaendeleo. Sana sana kinachoweza kujitokeza ni kuwatumia vijana pale wanapohitajika kama vile kwenye shughuli za mwenge na zile ambazo ni za mikusanyiko ya muda kwa haja ya shughuli, ikiisha, basi kila kijana aende zake.

Mheshimiwa Spika, haiwezekani kurugenzi ya vijana wizarani ikawa chini ya mtu mwenye umri zaidi ya vijana. Ni dhahiri hataendana kitabia, kimaadili na kadhalika. Kubwa zaidi atakuwepo katika nafasi hiyo ili tu kutimiza matakwa ya mwajiri.

Mheshimiwa Spika, Asasi za nje kama *Pan Africa Youth Union*, Mratibu wake umri umemruka, anastahili kustaafu na nafasi hiyo ishikiliwe na kijana mwenye uwezo wa kuwakilisha maslahi ya vijana. Umri kama wa huyo mratibu ni dhahiri umefika kujiwakilisha yeze zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na watendaji vijana, hii ni *special* kwa eneo hili la vijana eneo la ajira na kazi yafuate mtiririko wa kiwizara, lakini eneo la vijana liwe la vijana, hapo utaona changamoto inakuwepo na msukumo wa vijana kwa shughuli za maendeleo utakuwa mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri katika nchi yetu kuna makundi mawili makubwa ya wakulima na wafanyakazi. Pengine eneo lingine ni la wafanyabiashara. Ukiiondoa kundi la wakulima na wafanyabiashara utabaki na wafanyakazi. Eneo kubwa la wafanyakazi ni ajira. Ni muhimu Wizara ikawa karibu sana na eneo la wafanyakazi kama hatua za kuiondolea migogoro ya mara kwa mara nchi. Maeneo ya ajira ya kupewa kipaumbele ni kama:-

- Suala la mikataba kati ya waqajiri na waajiriwa;
- Mishahara inayotolewa inalingana na hali ya uchumi wa nchi?;
- Udhalilishaji/ynyanyasaji kuzingatia muda wa kazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, misingi ya nchi yetu kulingana na idadi ya watu, ni dhahiri ajira hazitoshelezi katika utaratibu huo, sekta isiyo rasmi ndio imeshauri eneo linalomilikiwa na *Enterprenuer* (wajasiriamali), lakini eneo hili limezingatiwa na kuendelezwa kwa kiwango kipi, inasikitisha kuona hadi sasa wajasiriamali wadogo wadogo bado wananyanyasika pale wanapohitaji elimu, mkopo na hata nyenzo mbalimbali za kumwendeleza. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie eneo hili kwa macho mawili kwa Mikoa yote ya Tanzania na Wilaya zake. Pia naomba sasa Wizara iwe na Afisa vijana kwa kila Wilaya ili aweze kuratibu maendeleo ya vijana na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Iramba Magharibi tunazo (MWMA-KI), Jipe Moyo – Shelui, Chamwai Ndogo *SACCOS* na kadhalika bado *SACCOS* hizi zinahitaji kuwezesherwa kiuwezo (*capacity building*) ili zifanye vizuri zaidi. Namwomba Mheshimiwa Waziri atoe mtaalam ambaye atawajengea uwezo.

Mheshimiwa Spika, *NMB* Kiomboi ilikuwa wakala wa fedha za wajasilamali 2006/2007 kwa bahati mbaya haikufanya vizuri sana kuzuia mikopo ya takribani

Sh.500,000/= ndio ilitolewa. Nashukuru sasa Meneja wa *NMB* na Afisa Mikopo walihamishwa kwa sababu hii. Sasa nasikia Asasi ya *Pride* ndio imechua nafasi yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri afahamu kwamba *Pride* haipo Iramba, ipo Singida Mjini. Aangalie, kwa sababu inawezekana wajasiriamali wa Iramba wasipewe mikopo. Naomba utaratibu uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana *NSSF* chini ya Mkurugenzi wake Dr. Dau kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX KIJKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wake kwa hotuba nzuri ambayo imeandikwa kwa kitaalam. Kutokana na umahiri wao huo, napenda kusema kuwa ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja, napenda kutoa mchango wangu mdogo katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi zinafanywa na *NSSF* ni za uhakika na hasa kwa kufanya kazi ambazo zinakwenda sambamba na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Ninashauri la kwamba kuwa katika jihada za Serikali kufungua uchumi wa Mkoa wa Kigoma, basi Shirika hilo lipewe nafasi ya kujenga majengo kadhaa Makao Makuu ya Wilaya ya Kibondo, nyumba ambazo wananchi na hasa watumishi wataishi kwa mtindo wa kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa hapo Kibondo wanaishi kwenye nyumba ambazo hazina hadhi na salama. Naomba sana msaada huo wa *NSSF* au *PPF* kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, bado fedha za JK ambazo zinasaidia vikundi hazikuwafikia wananchi wa Kibondo. Sasa hivi viro vikundi 37 ambavyo vimeundwa kwa ajili ya kupata mkopo wa fedha hizo ili ziweze kuchangia kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa makusudi mazima yatolewe mafunzo maalum kwa Maafisa wa Ushirika nchini hususani katika usimamizi na uanzishaji wa vikundi hivi vyta wajasiliamali.

Aidha, *TIRDO* na *SIDO* ni maeneo muhimu ambayo yana uwezo mkubwa wa kuanzisha miradi kwa vijana na wananchi kwa ujumla ili kujitegemea. Sekta hizi mbili zinao uwezo mkubwa wa kubuni miradi ambayo inaweza ikawa changamoto.

Mheshimiwa Spika, ninaomba itungwe sheria inayosimamia mafao kwa watu wanoumia kazini. Kiasi cha fedha kinachotolewa hakitoshi.

**MHE. MARIA IBESHI HEWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza hotuba hii kwa sababu inaonyesha mwelekeo katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, Shirika La NSSF; awali ya yote, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Shirika hili kwa juhudzi za utekelezaji wa malengo mbalimbali kwa mfano ujenzi wa majengo, vyuo, shule, ofisi na kadhalika ukiwemo mji wa Mwanza. Hoja yangu ya kuuliza ni lini ujenzi wa Banda/Jengo la Machinga linalotegemewa kujengwa Mwanza litaanza? Je, vibali na michoro iko tayari? Wamachinga hao wana taarifa? Nauliza hivyo kwa ajili ya maandalizi ili kasi ya ujenzi isikwame eti hawajaandaliwa. Naomba ufanuzi katika majumuisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira milioni moja, napenda niipongeze Wizara angalau kwa kuipata takwimu hiyo ya idadi ya ajira zilizopatikana tangu tamko la Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la idadi ya ajira bado kunahitajika ambalo sio chini ya Laki sita, idadi hiyo inapashwa kuwa katika lengo – kwamba katika kila mwaka tuwe na kutafuta ajira hizo. Hapo ndipo lengo tutalikamilisha au hata kuzidi. Maeneo yabainishwe haraka kwa mfano Mjini na vijiji maeneo kama mahotelini, viwandani na hata wanaojajiri katika sekta ya kilimo.

**SPIKA:** Sasa nitamwita mtoa hoja ili aweze kuendelea, lakini kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri wa Kazi nilikuwa nataka kusema kwamba Wizara inayofuata ni Wizara ya Kilimo, lakini kwa jinsi ilivyopangwa, hili limekuja kama ghafla kidogo, hatutaweza kuanza saa 11.00, tutaendelea hivyo hivyo kama ilivyopangwa kwamba Wizara ya Kilimo ni kesho baada ya maswali.

Nakumbushwa na Mheshimiwa John Cheyo kwamba wenye mawazo yoyote kuhusu *CDF*, Wabunge wowote sio wale tu walio kwenye Kamati, Kamati itapokea maoni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana mkutano unafanyika pale saa 7.30 katika Ukumbi wa Pius Msekwa kwa sababu hiyo na Mheshimiwa Lubeleje anathibitisha hilo hilo, Wabunge wowote ambao wanapenda kusikiliza au kutoa maoni kuhusu harakati za kuwezesha *CDF* ipatikane basi fursa yao ni hapo saa 7.30.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ni dhahiri kwamba baada ya kuahirisha tutakopomala shughuli za Wizara hii ya kazi, basi pengine itabidi nitangaze kuwa tunaahirisha hadi kesho lakini hatua hiyo hatujaifikia. Ngoja twende na haya yaliyopo mbele yetu. Kwa hiyo, kwa heshima na taadhima sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa muda usiozidi dakika 60 ili aweze kujibu hoja mbalimbali na kutoa ufanuzi wa hoja za Waheshimiwa Wabunge na utusaidie kujibu swali la Spika kwamba kwa nini NSSF hawaendi kabisa Urambo. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge nikianza na hii hoja ya kwa nini NSSF hawaendi Urambo kabisa. Nina hakika

baada ya kusikia kauli yako na Waziri atatia nguvu hapo hapo, *NSSF* wamesikia na watatutembelea Urambo kuja kuangalia ambayo tunaweza kushirikiana nao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa kwa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii kupidia kwa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mbunge wa peramiho. Ushauri wa Kamati umekuwa ni wa kina na umeyachambua na kusisitiza maeneo kadhaa kwa kutoa maelekezo mbalimbali ili kuongeza ufanisi wa Wizara na Taasisi zake. Kamati pia imesaidia sana katika kusukuma mambo ya msingi ndani ya Serikali ili kuharakisha maamuzi yakiwemo masuala ya daraja la Kigamboni.

Pia napenda kutoa shukrani za dhati kwa maoni na ushauri uliotolewa na Kambi ya Upinzani kupidia kwa Msemaji wake Mkuu wa Wizara yangu - Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan, Mbunge wa Tumbe.

Kwa hakika naomba nikiri kwamba, mchango wa safari hii umekuwa na lengo la kuboresha Wizara na Taasisi zake. Sio kukosoa kwa maana ya kupinga tu kama tulivyokuwa tumezoea huko nyuma. Namshukuru sana Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan na namwahidi kuwa maoni na ushauri wake tutayafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, jumla ya Wabunge 18 walichangia kwa kuzungumza na 32 wamechangia kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge 16 walichangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi, tunaahidi kuwa tutazingatia yote kwa lengo la kufanikisha majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge walionipongeza, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara na Wakuu wa Mashirika na Taasisi zao zilizo chini ya Wizara yangu. Pongezi zao zimetupa moyo wa kufanya kazi kwa bidii zaidi. Napenda kutoa sahihisho moja tu, mimi ni Mbunge wa Urambo Magharibi na sio Urambo Mashariki kama ilivyoripotiwa katika baadhi ya magazeti.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii pia kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa wote waliotenga muda wao na hatimaye kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi na wengine kwa kuzungumza. Hakika michango yao imekuwa ni ya umahiri wa hali ya juu sana na imeonyesha ukaribu walionao kwenye shughuli za Wizara yangu na Taasisi zake. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kuwa mahusiano ya aina hii yanatutia faraja kwa kuona kuwa tuna wenzetu amba daima watatusaidia kutuelekeza kwenye njia sahihi amba watatusaidia katika kuwatumikia Watanzania amba ndiyo waliotuleta humu ndani ili kuwajengea matumaini ya maisha bora kwa kila Mtanzania. Kwa ushirikiano wa namna hii tunaufanya ule mzigo mzito kuwa mwepesi kwa sababu tunagawana. Sisi kama Wizara na Taasisi zake tunachukulia michango yenu kama ni nyenzo muhimu katika utendaji wetu wa kazi ili kuiwezesha Wizara yetu kuwa na ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa, naomba kwa ruhusa yako, niwatambue kwa majina Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hotuba yangu. Waheshimiwa waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa James Phillip Musalika, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mheshimiwa Paul Peter Kimiti, Mheshimiwa Bujiku Phillip Sakila, Mheshimiwa Profesa Raphael Benedict Mwalyosi, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Dr. Harrison George Mwakyembe, Mheshimiwa Jacob Dalali Shibili, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir na Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Dr. Luka Jelas Siyame, Mheshimiwa JUma Hassan Kilimbah, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Sijapata Fadhili Nkayamba, Mheshimiwa Kanal Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Mohammed Said Sinani, Mheshimiwa Ali Ameir, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya na Mheshimiwa Suzan Anselim Jerome Lyimo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifan, Msemaji wa Kambi ya Upinzani; Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mheshimiwa Monica Ngezi Mbega, Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Engineer Stella Martin Manyanya, Mheshimiwa Janeth Moris Massaburi, Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Ibengwe Mongella, Mheshimiwa Thomas Abson Mwang'onda na Mheshimiwa Said Juma Nkumba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge waliochangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Fedha na Uchumi ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zuberi, Mheshimiwa Abbas Mtemvu, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, Mheshimiwa Erasto Weston Zambi, Mheshimiwa Juma Njwayo, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Elieta Switi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelili, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mheshimiwa Margareth Mkanga na Mheshimiwa James P. Musalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako sasa napenda nianze kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizotolewa katika kuchangia Hoja ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Naanza na Idara ya Kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwanza ilikuwa Serikali ilifanyiwe utafiti wa kina suala la kima cha chini cha mishahara katika Sekta Binafsi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii. Ushauri huu umezingatiwa kikamilifu. Serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam *Economic Research Bureau* ipo katika hatua za mwisho kukamilisha utafiti huo kuhusu kima cha chini cha mishahara ili kujua athari. Utafiti huo utakamilisha mwishoni mwa mwezi Agost, 2008. Lengo ni kuweka mfumo bora wa uwekaji kima cha chini cha mishahara katika Sekta Binafsi ambao pia utazingatia umuhimu wa kuoanisha mishahara hiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ilikuwa Serikali ihakikishie wafanyakazi katika Sekta Binafsi wanalipwa mishahara kupitia Benki ili wote waweze kulipa kodi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Abbas Mtemvu. Sheria za kazi hazilazimishi waajiri kuwalipa mishahara kupitia Benki. Hata hivyo, jambo hili linawezekana kupitia makubaliano kati ya waajiri na wafanyakazi. Aidha, kwa mujibu wa Sheri za Kodi, mishahara yote inayostahili kukatwa kodi hupaswa kukatwa kodi bila kujali endapo itakuwa imepitia Benki au vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tatu, ilikuwa Serikali iangalie upya utaratibu wa kuwa na mikataba ya ajira kwa wafanyakazi ili kunufaisha wafanyakazi na kupunguza migogoro katika sehemu za kazi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Said Nkumba. Katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote wanakuwa na mikataba ya ajira yenye kuwanufaisha, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Moja, imeandaa mkakati maalum wa kutoa elimu kwa wafanyakazi kuhusu sheria mpya za kazi pamoja na mambo mengine. Msisitizo wa mafunzo hayo ni kuwaelimisha waajiri na wafanyakazi kuhusu wajibu na haki zao ikiwa ni pamoja na uundaji wa Mabaraza ya Wafanyakazi. Pili, imeanzisha Kitengo Maalum kwa ajili ya kufanya ukaguzi katika sehemu za kazi. Lengo ni kubaini baadhi ya waajiri wakorofii wasiotaka kuzingatia sheria na kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne, Vyama vya Wafanyakazi viweke mikakati kuelimisha wafanyakazi kuhusu sheria za kazi ili kuwawezesha kujua taratibu za kushughulikia migogoro sehemu za kazi. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Pindi Chana.

Mheshimiwa Spika, Vyama vya Wafanyakazi vinaendesa programu ya kuwaelimisha wanachama wao kuhusu sheria mpya za kazi inayoelekeza utaratibu mzima wa kuzuia migogoro na haki zao katika sehemu za kazi. Pia Serikali na Shirika la Kazi Duniani *ILO* zinasaidia kutoa elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano, Wizara ishughulikie mara moja malalamiko ya wafanyakazi ili kuepusha migogoro katika sehemu za kazi. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Juma Killimbah na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. Wizara katika kulizingatia hilo ina mkakati wa kuimarisha kaguzi sehemu za kazi na kutoa elimu kuhusu sheria mpya za Kazi. Pia kuna chombo maalum kimeundwa, Tume ya Usuluhishi na Uamuzi, yaani *Commission for Mediation and Arbitration* kinachoharakisha suluhishi na utatuzi wa migogoro kama nilivyoeleza katika hotuba yangu. Kwa utaratibu huu migogoro inachukua wiki tatu tu kumalizika.

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita, ilikuwa sheria ya fidia kwa wafanyakazi imepitwa na wakati. Hii hoja imetolewa na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani na Mheshimiwa Said Nkumba. Serikali inatambua kuwa sheria hii imepitwa na wakati na viwango vya malipo vinavyotolewa kwa mujibu wa sheria hii havilingani na madhara halisi yatokanayo na ajali au magonjwa. Kwa mfano, mtu akifariki analipwa Sh. 80,000/=, ukiumia na ukaonekana kwamba umeathirika asilimia 100 unalipwa Sh. 108,000/=, kwa kweli hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hali hii Serikali imekamilisha Muswada wa Sheria mpya ya fidia na utarajiwa kujadiliwa na Bunge lako Tukufu katika vikao vijayvo vya hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, hoja ya saba, ilikuwa Elimu ya *UKIMWI* imetolewa kwa wafanyakazi. Hoja hiyo imetolewa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa Luka Siyame. Fasihi ya Maadili kuhusu *UKIMWI HIV/AIDS Code of Conduct* itakayotumika kama mwongozo wa kutoa Elimu ya *UKIMWI* katika sehemu za kazi imekamilika na ipo katika hatua za uchapishaji, mara itakapokuwa tayari elimu itaanza kutolewa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nane, kero za wafanyakazi wa Shirika la Posta imetolewa na Mheshimiwa Said Nkumba. Wizara imepokea kero za watumishi hao na itafuatilia kwa karibu ili kupata ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tisa, aina ya mikataba ya ajira kwa wafanyakazi ifafanuliwe. Hii hoja ilitolewa na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi. Kwa mujibu wa sheria ya ajira na mahusiano kazini Na.6 ya mwaka 2004 kuna aina tatu za mikataba ya ajira. Aina ya kwanza ni mikataba usioonyesha muda maalum. Mkataba wa aina hii hauonyeshi tarehe ya ukomo. Kwa lugha ya kawaida ambayo tumezoea ni kama vile umepata ile kazi ya kudumu au *permanent*. Aina ya pili ya Mkataba, ni mikataba unaonyesha muda wa ukomo kwa kada ya wataalam na meneja. Mkataba wa namna hii huwezi kuvunjwa bila ya sababu maalum. Aina ya tatu ya mikataba, ni mikataba wa kazi maalum na mikataba wa namna hii unategemeana na kwisha kwa kazi au shughuli husika. Kwa mfano, mtu anakujengea nyumba, una uhakika nyumba hiyo itachukua miaka miwili, basi mnapeana mikataba wa miaka miwili, kazi ikiisha na yeye mikataba umekwisha.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi, mgogoro wa wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari *TPC* Moshi kuhusu kufukuzwa kazi tarehe 24 Aprili, 2008. Kimsingi Wizara yangu haina taarifa za kufukuzwa kazi kwa wafanyakazi 168 wa *TPC* tarehe 24 Aprili,

2008. Wizara ina taarifa za mgogoro wa Said Kitundu na wenzake 149. Mgogoro uliosajiliwa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi Moshi, 2007, Mgogoro Namba MS/CMA/ARB/04/2007 uliosikilizwa na kutolewa maamuzi. Katika mgogoro huo wafanyakazi walishindwa na hakuna taarifa za wafanyakazi hao kupinga maamuzi ya Mahakama ya Kazi sehemu ya Mahakamu Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina taarifa mgogoro wa Jastini Samwel na wenzake watatu uliofunguliwa Tume ya Usuluhishi ya Uamuzi Moshi, Mgogoro Namba 1/CMA/ARB/97/2007, wafanyakazi hao wanawakilishwa na Wakili Msomi Materu, shauri litaendelea kusikilizwa tarehe 22 Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na moja inahusu uhuru wa wafanyakazi kujiunga katika Vyama Uhuru vya Wafanyakazi. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Kabwe Zitto na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Serikali inatambua na kuheshimu uhuru wa wafanyakazi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi. Mgogoro kuhusu ni Chama kipi kiwakilishe wafanyakazi katika Kiwanda cha Sukari *TPC* Moshi uliwasilishwa na wafanyakazi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Vyama vilivyohusika katika mgogoro huo ni *TIPAO* na *TWICO*, Mahakama ilitupilia mbali shauri hilo kwa kuwa haikuwa na mamlaka ya kusikiliza badala yake ilielekeza shauri hilo liwasilishwe katika Mahakama ya Kazi. Uamuzi huo ulithibitishwa na Mahakama Kuu Moshi. Wafanyakazi wanafanya utaratibu za kuwasilisha rufaa yao katika Mahakama ya Rufaa Tanzania. Aidha, kumbukumbu zilizopo zinathibitisha kuwa Chama cha *TWICO* wamejitoa kabisa katika suala zima la uwakilishi wa wafanyakazi wa *TPC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chama cha Tanzania *Social Service Industrial Workers Union TSSIWU* ni kweli kuwa kwa mujibu wa Katiba yao hawajaruhusiwa kuwakilisha wafanyakazi katika Kiwanda cha *TPC*. Ni kweli pia kuwa *TSSIWU* pamoja na Vyama vingine vilivyo sajiliwa walielekezwa kuzifanyia marekebisho Katiba zao ili zikidhi matakwa ya vifungu vya 46 na 47 vya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazi Na.6 ya mwaka 2004 na kuwasilisha kwa Msajili wa Vyama. Chama cha *TSSIWU* walitekeleza agizo hilo kwa kuwasilisha Katiba yao yao mwezi Juni na Katiba hiyo inafanyiwa kazi na msajili ili kubaini iwapo marekebisho hayo yanakidhi haja ya Chama hicho.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha waajiri kuwazuia wafanyakazi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Wafanyakazi ni kosa kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na.6 ya mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, walioathirika vitendo hivyo wanapaswa kuwasilisha malalamiko yao katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi. Isitoshe Elimu kuhusu Sheria mpya za kazi inaendelea kutolewa na Serikali pamoja na wadau wake ili kuwawezesha wafanyakazi na waajiri kufahamu vyema wajibu na haki zao.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na mbili, mwaliko wa Mheshimiwa Waziri kutembelea sehemu za kazi kiwanda cha samaki Musoma na Kiwanda cha Nyuzi Tabora ili akutane na wafanyakazi na kujadiliana nao kuhusu haki zao kwa mujibu wa sheria za

kazi. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally.

Ninataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba mwaliko umekubaliwa, taratibu zitafanywa ili ziara hiyo iweze kufanyika na masomo kuhusu Sheria mpya za kazi kutolewa. Labda swali ni kwamba, sijui Mheshimiwa Waziri atapata bahati ya kusindikizwa na Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja katika kila sehemu yake, itakuwa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na tatu, migogoro ya wafanyakazi kuhusu kutokulipwa mafao ya kuachishwa kazi katika Kiwanda cha Mbeya cha Sementi na Mbeya *Industries*. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda. Wizara yangu haijapokea madai ya wafanyakazi kutoka katika Kiwanda cha Mbeya Sementi na Mbeya *Industries*. Wizara itafuatilia kujua aina ya madai ya wafanyakazi hao na kutoa ushauri ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na nne, mgogoro wa wafanyakazi wa *AMI Kigoma, Tanzania Ports Authority* na *SPM Mgololo*. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Madai ya wafanyakazi *AMI Kigoma* yapo katika Mahakama ya Kazi na uamuzi bado kutolewa. Kuhusu madai ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Mgololo madai hayo yamekwishatolewa maamuzi na Mahakama ya Kazi kuwa walipwe haki zao na mwajiri wao. Madai ya wafanyakazi *Tanzania Ports Authority* yanaendelea kusikilizwa na Tume ya Usuluhishi na Uamuzi *CMA*.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na tano, mgogoro wa wafanyakazi wa Kampuni ya Vikishishi Mwanza kuhusu kupunguzwa kazi. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi. Vijana waliokuwa wanafanya kazi katika kiwanda cha Vikishishi walipunguzwa kazi kutokana na mwajiri kufunga baadhi ya vitengo walivyokuwa wanafanya kazi kama vile mgahawa, Karakana, Ulinzi na bustani na kuingia mkataba na watu wa nje (*outsource*). Kwa mujibu wa sheria mpya za kazi shauri hili linashughulikia na Tume ya Usuluhishi na uamuzi Kanda ya Mwanza na limepangwa kuendelea kusikilizwa tarehe 4 Agosti, 2008.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na sita inahusu Mifuko ya Hifadhi za Jamii iweke utaratibu wa kuwawezesha wanachama kukopa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Lucas Selelii. Jambo hili limezingatiwa katika Sheria ya Mamlaka na Udhhibit na Usimamizi wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii, yaani the *Social Security Regulatory, Authority Act*, 2008 iliyopitishwa hivi karibuni na Bunge. Kwa mujibu wa sheria hii mwanachama ataruhusiwa kutumia sehemu ya malimbikizo ya michango yake kama dhamana ya kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba.

Mheshimiwa Spika, sasa naingia katika Idara ya Ajira. Hoja ya saba iliyojitokeza ni changamoto kuhusiana na ajira milioni moja na kama zitafikiwa kwa kasi ya sasa.

Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani - Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Said Arfi na Mheshimiwa Elietta Switi.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba ajira milioni moja zitafikiwa hasa kwa kuzingatia mafanikio ya malengo ya MKUKUTA. Wakati tunaanza mchakato wa namna ya kupata hizo ajira milioni moja, Wizara yangu iliwasuhisha wadau wote zikiwemo Wizara, Taasisi za Serikali, Mashirika Binafsi na Taasisi za Kimataifa ili kuweza kuwa na mpango au Mkakati Maalum wa kukusanya na kuwasilisha taarifa na takwimu za ajira mpya zinazozalishwa kwenye maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, Wizara kwa kushirikiana na *ILO* na *UNDP* iliweza kutayarisha programu ya Taifa ya Kukuza Ajira mwaka 2007 na kwa kuzingatia programu hiyo endapo wadau wote watashiriki zinaweza kuzalishwa ajira mpya milioni tano katika kipindi hiki na hivyo kupunguza ukosefu wa ajira kwa kiwango cha malengo ya *MKUKUTA*. Kwa hivi sasa bado ukusanyaji wa taarifa za ajira mpya unaendelea kwa kushirikiana na Ofisi ya Takwimu ya Taifa. Tuna imani kwamba utakapokamilika idadi ya ajira mpya mbalimbali zitakuwa zaidi ya 437,205 tulizotolewa taarifa kwa kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na nane, Serikali ina Mpango au Mkakati gani wa Ukuza wa Ajira Nchini hususan kwa vijana kwa kuhusisha wadau wengine. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir na Mheshimiwa Maria Hewa.

Mheshimiwa Spika, tayari Serikali imepitishwa Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2008 na Mkakati wa Ukuza wa Ajira Nchini umetayarishwa ambao utahusisha wadau wote na kuelezea majukumu yake yao katika kufikia lengo la kuongeza ajira na kupunguza umaskini husasun vijana ikizingatiwa kwamba suala la ajira ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kumi na tisa, ni vijana wangapi walio na uwezo wa kufanya kazi na walioajiriwa au kujiajiri hapa nchini. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo. Matokeo ya utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi mwaka 2006 yalionyesha kwamba ni jumla ya vijana 10,454,894, waliokuwa na uwezo wa kufanya kazi kati ya vijana wote 11,772,218 waliokuwepo nchini mwaka huo. Vijana walioajiriwa au kujiajiri ni 9,056,218, wanaume 4,264,151 na wanawake ni 4,792,067.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2006 kiwango cha ukosefu wa ajira kwa vijana kilikuwa ni asilimia 13.4, Mijini walikuwa na wastani wa asilimia 26.7 na vijini walikuwa na wastani 7.9.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini inahusu Mpango au Mkakati gani umeandalisha kwa ajira za watu wenyewe ulemavu. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Margreth Mkanga na Mheshimiwa Al-Shymaa Kwegyir.

Mheshimiwa Spika, katika Sera ya Taifa ya Ajira ya Mwaka 2008 Wizara imeainisha mpango wa kuwashirikisha watu wenyewe ulemavu katika ajira kwa kufuata Sera ya Taifa ya wenyewe Ulemavu. Aidha, mkakati wa ukuzaji wa Ajira Nchini umezingatia suala la makundi ya maalum yakiwemo ya watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na moja, kigezo cha uzoefu kwa wahitimu wa mafunzo katika kuajiriwa. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara yangu na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda.

Mheshimiwa Spika, tunakiri kwamba suala hili bado ni changamoto kwetu, tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu kutusaidie kuweka msisitizo wa kutoa elimu kwa kuzingatia mafunzo ya vitendo pia ili iwe rahisi kwa wahitimu kupata ajira na kutazama uwezekano wa kuwapitisha wahitimu hao wa Vyuo katika sehemu za kazi ili wapate uzoefu. Aidha, tunatoa wito kwa waajiri kuititia Vyama vyao walitazame tatizo hili na kukubali kuwapokea wahitimu wetu na kuwawezesha kupata uzoefu kabla hajaingia katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na mbili, namna ya kutambua ajira za wataalam wenyewe ujuzi maalum kama vile marubani. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. Kama nilivyosema katika hotuba yangu, Wizara itakamilisha maandalizi ya Kamusi mpya ya Kazi ya mwaka 2008/2009 ambayo itatuwezesha kufahamu idadi ya nafasi za wataalam hapa nchini katika fani mbalimbali zikiwemo za marubani.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na tatu, vibali vya ajira za wageni katika Kampuni za simu. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Vigezo vinavyotumika kutoa vibali vya kazi kwa wageni kutoka nchi za nje ni kuhakikisha kwamba mgeni anayekuja kufanya kazi hapa nchini anakuja kufanya kazi ambayo hakuna Mtanzania anayeweza kuifanya. Wawekezaji kuititia *TIC* wanaruhusiwa kuwa na idadi ya wageni watano au zaidi kutokana na ukubwa wa shughuli zao. Hivi sasa Wizara inaendesha zoezi la ukaguzi wa makampuni yote yaliyoomba vibali kuititia Wizara yangu pamoja na mambo mengine kutazama mfumo mzima wa namna ya ulipwaji mishahara na kubaini wageni wanaofanya kazi kinyume cha taratibu.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kuititia mradi wa *BEST* ina mpango wa kumpata mshauri mwelekezi atakayefanya utafiti na kushauri namna ya kuboresha utaratibu mzima wa utoaji wa vibali vya kazi kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na nne, halafu vilevile kulikuwa na suala la uanzishwaji na mafanikio wa Vituo vya Ajira. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa na Mheshimiwa Faida Bakar. Lakini vilevile kulikuwa na suala ambalo Mheshimiwa Pindi Chana ameliuliza ambalo linahusiana na Vituo vya Ajira nchini ambapo amesema ipo haja ya kuunganisha watafuta ajira na waajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza hapa nchini Kituo cha Ajira kilianzishwa mwezi Julai, 2001 katika Jiji la Dar es Salaam kwa msaada wa Serikali ya Marekani. Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa Vituo hivyo vinafunguliwa katika nchi nzima kwa Kanda na kwa hivi sasa tumeanzia Kanda ya Ziwa Mwanza na baadaye tutajenga Kanda ya Kusini Magharibi, Kati na Kaskazini. Mafanikio yaliyopatikana kuanzia mwaka 2001 hadi hivi sasa ni kuandikisha watafuta kazi 13,073 na kuwaunganisha vijana 7,682 kwa waajiri katika Jiji la Dar es Salaam ambao kati yao wanaume 4,732 na wanawake ni 2,950.

Mheshimiwa Spika, tangu Kituo cha Mwanza kianzishwe mwezi Mei, 2007 kimeandisha watafuta kazi 405 na kuunganisha vijana 243 kwa waajiri, kati yao wanaume ni 169 na wanawake ni 74.

Hoja ya ishirini na tano, uboreshwaji wa Jengo la Uwakala wa Huduma za Ajira Nchini TAESA pamoja na maslahi ya wafanyakazi. Suala hili limeulizwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi. Tumeupokea ushauri huo na tutauzingatia katika utekelezaji wa malengo na mipango ya Wakala TAESA kwa kuanzia na uboreshaji wa jengo, maslahi ya wafanyakazi pamoja na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha Wizara ipo katika mpango wa kufungua Ofisi za Kanda ya Kusini Magharibi na Kaskazini katika Mikoa ya Mbeya na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na sita ni ufanuzi kuhusu Mfuko wa Dhamana *Revolving Loan Fund* wa Mradi wa Usawa na Jinsia na Ajira Bora kwa Wanawake. Hili limeulizwa na Mheshimiwa Shally Raymond. Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2001 na *ILO* kwa kushirikiana na Serikali na Wadau wa Utatu kwenye Mikoa ya Tanga Manispaa ya Muheza, Mbeya Tukuyu, Dar es Salaam Manispaa zote Tatoo, Unguja na Pemba. Mradi huu unalenga kuboresha ajira kwa wanawake waliojiajiri wenye kwenye sekta isiyo rasmi na vijana waliopo kwenye kazi hatarishi pamoja na kukomesha ajira ya watoto. Mfuko huu unatoa mikopo kupitia *SACCOS* ya Wanawake kwenye maeneo ya miradi. Matarajio ya Serikali ni kuendeleza dhana hii kwenye maeneo mengine ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na saba inahusu Mfuko wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi JK *Fund*. Hoja zilizowasilishwa kuhusu Mpango wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi JK *Fund*, uchache wa fedha za mkopo na wananchi wengi kutofikiwa vijijini. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Dr. Lukas Siyame, Mheshimiwa

James Musalika, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Said Arfi, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Vita Kawawa, Mheshimiwa Kanal Feteh Saad Mgeni na Mheshimiwa Lekule Laizer.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa fedha shilingi bilioni 10.5 zilitengwa kwa mpango huo wa Awamu ya Kwanza ni chache sana kuliko mahitaji ya wajasiriamali. Kwa mfano, idadi ya maombi yaliyopokelewa na *NMB* yalikuwa ni wajasiriamali 92,263, maombi hayo yalikuwa na thamani shilingi bilioni 165.6, lakini mikopo ilitolewa kwa wajasiriamali 21,135 tu kati ya wajasiriamali 92,263, yenye thamani ya shilingi bilioni 16.1 na waliopata mikopo ni sawa na asilimia 22.9 hali kama hiyo imejitokeza pia kwa Benki ya *CRDB*.

Mheshimiwa Spika, tunachojaribu kuonyesha hapa ni uwiano ambao si chanya, tuseme siyo *positive*. Kwa sababu waombaji ni wengi sana lakini na fedha ni kidogo ili fedha ziweze kuwafikia wengi zaidi tutasisitiza na kuimarisha urejeshaji wa fedha zinazorejeshwa zikopeshwe tena kwa wengine kwani fedha hizo ni za mzunguko. Sasa tatizo hapa ni kwamba kama fedha hizo zingerejeshwa zote kwa wakati unaotarajiwa ni kwamba ziweze vilevile kuwafikia wengine zaidi pengine baada ya kuzungumza watu 21,000 tungejikuta tunazungumzia watu 42,000. Kwa hiyo, tatizo lipo katika urejeshaji.

Mheshimiwa Spika, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa kushirikiana na Serikali katika kuhamasisha wananchi kurejesha mikopo waliochukua kwa wakati ili wananchi wengine waweze kukopa. Awamu ya pili, imelenga kurekebisha upungufu uliojitokeza katika awamu ya kwanza kwa kuelekeza fedha za mikopo kwenye maeneo ya vijijini kwa kutumia Asasi za Fedha zenye uzoefu wa kutoa huduma ya mikopo vijijini kama vile *SCCULT*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuyafikia maeneo ambayo hayakufaidika na mikopo katika awamu ya kwanza, tayari Serikali imekwishatoa maelekezo kwa Benki Kuu kutoa fedha kwa ajili ya wajasiriamali wa maeneo ya vijijini ambayo hayakufikia ikiwemo Jimbo la Nyang'hwela la Mheshimiwa James Musalika.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile, hoja ya Mheshimiwa Lekule Laizer kuhusu zile Wilaya za wafugaji, nalo pia Serikali imekwishalitolea maagizo kwenye Benki Kuu ili waone namna ambavyo wanaweza wakazihamisha fedha zile ziweze kuelekezwa katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, tunayo vilevile hoja ya wananchi kutoka Wilaya ya Kibaha. Pale kuna Halmashauri mbili, Halmashauri moja ilichukua fedha zote ikatumia na Halmashauri nyingine ikakosa, hilo nalo tutazingatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha kuitishwa kwenye *SACCOS* moja kwa moja, inategemea na *SACCOS* husika na Asasi nyingine kukidhi masharti ya Benki Kuu. Kwa msingi huo tunawashauri Waheshimiwa Wabunge ikiwa kuna Asasi katika maeneo yao

ambazo zinaweza kutoa huduma za mikopo kuwasilisha majina ya Asasi hizo kwa Uongozi wa Mkoa na Wilaya ambao utawasilishwa Benki Kuu kwa tathmini.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini na nane, fedha za wajasiriamali kutolewa kwa wasiotarajiwa. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Monica Mbega, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Jacob Shibiliti.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kutoa mikopo ulikuwa wa wajasiriamali wanawasilisha maombi kwenye Ofisi za Vijiji au Mtaa kwa utambulisho na uhakika wa mwombaji. Kisha maombi yanawasilishwa kwenye Kamati ya Kata kwa ajili ya kuhakikiwa na kuitishwa kulingana na vipaumbele vya Kata. Vigezo vya vipaumbele vinawekwa na Kamati ya Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya walengwa hawakupata mikopo kwa sababu kadhaa ikiwemo baadhi za Kata na Wilaya kutozingatia utaratibu wa vipaumbele vilivyowekwa Kiwilaya au kwa vile mpango huu ulikuwa mgeni kwa wahusika wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Benki ya *NMB* mikopo ilikuwa inatolewa ndani ya umbali wa kilomita 20 tu toka lililopo Tawi hilo, hivyo kuishia kuwahudumia wananchi wa Mijini zaidi. Kiambatanisho namba tano kwenye hotuba yangu kinaleza hiyo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya ishirini tisa, riba kubwa na muda wa kurejesha mikopo mfupi mno kwa miradi ya kilimo. Swali hili limeulizwa na Mheshimiwa Shally Raymond na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe. Riba ya mikopo chini ya mpango huu ni asilimia 10 kwa mwaka. Aidha, *SACCOS* zimeruhusiwa kuongeza kiwango kisichozidi asilimia mbili kwa ajili ya gharama za uendeshaji. Kiwango hiki kina riba cha chini kuliko kile cha mabenki na Asasi nyingine. Hofu yetu sisi ni kwamba ukizidi kupunguza riba hii inaweza kuathiri mpango wa kuwawezesha wajasiriamali hatimaye kuingia kwenye mfumo wa kawaida ya mikopo ya benki.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba na mabenki muda wa marejesho wa mkopo hauzidi miaka mitatu, hivyo miradi ya kilimo inapaswa pia kunufaika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya thelathini, umuhimu wa utoaji mafunzo kwa wajasiriamali hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Maida Hamad, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Dr. Luka Siyame na Mheshimiwa Diana M. Chilolo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali kabla na baada ya kutoa mikopo ni suala la msingi na lenye kuboresha malengo ya mpango na tija kwa wajasiriamali. Ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kuhusu hili utazingatiwa. Aidha,

benki na asasi zote za fedha kwenye mpango huu zinawajibika kwenye mkataba kutoa mafunzo kwa walengwa kabla ya kuwapatia mikopo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya thelathini na moja, ilikuwa ni kutopatikana kwa taarifa na usiri wa kupata orodha ya wajasiriamali waliopata mikopo na hali ya marejesho. Hili limeulizwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi na Mheshimiwa Said Nkumba. Katika awamu ya kwanza benki za *CRDB* na *NMB* zilitakiwa kuwasilisha majina ya wajasiriamali wote waliokopa na kiasi walichokopa kwa Benki Kuu. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu tayari Wizara imepokea kutoka Benki Kuu orodha ya wajasiriamali wote waliopata mikopo kutoka Benki za *NMB* na *CRDB*. Orodha hii tayari tumeipanga kimkoa na tutawasilisha kwenye ofisi za wakuu wa Mikoa kwa ajili ya taarifa za ufuutiliaji. Aidha, tunawashauri Waheshimiwa Wabunge, wanaohitaji kuwajua waliokopa kuwasiliana na ofisi husika.

Mheshimiwa Spika, kwenye awamu ya pili, Serikali imekubaliana na Benki na asasi za fedha zinatoa mikopo kutoa taarifa za wakopaji na mwenendo wa urejeshaji Mikopo katika ngazi ya Mkoa na Wilaya ili viongozi waweze kufuatilia na kuwatambua waliokopa mikopo na kuhimiza urejeshaji mikopo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, halafu kuhusu Benki ya Kigoma kuajiri walinzi Warundi badala ya walinzi wa Kitanzania, ni swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Sijapata Nkayamba. Suala hili tumelipokea na tutalifuatilia ili kulitolea majibu.

Mheshimiwa Spika, hoja ya thelathini na mbili, ni ushauri kwamba tathimini ifanyike kubaini mafanikio ya matatizo pamoja na walionufaika na mikopo hiyo. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Salum Abdallah Khalfani, Mheshimiwa Janeth Massaburi na Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Baraza la Uwezeshaji wa wananchi na wadau wa mpango kuititia uongozi wa Mkoa na Wilaya itafanya tathimini ya kina ili kujua mafanikio yaliyopatikana pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa mpango huu. Tathimini hii imekwishaanza kufanyika kama tulivyosikia wote kutokana na agizo la Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, hoja ya thelathini na tatu, umuhimu wa kueneza mfumo wa vikoba kwenye maeneo mengine. Hoja hii imeletwa na Mheshimiwa Monica Mbega. Wazo hili ni zuri kwa sababu linawahamasisha wananchi wa hali ya chini kuwa na tabia kuweka akiba na kukopa ambaa ni msingi mzuri wa dhana ya ushirika na ujasiriamali.

Mheshimiwa Spika, aidha, vikoba vinaweza kujiunga na *SACCOS* na kunufaika na huduma za *SACCOS* zilizoko kwenye maeneo yao, hivyo tunakubaliana na wazo kuwa mfumo wa vikoba usambazwe nchi nzima na tutalifanya kazi wazo hili. Kweli kama alivyokuwa akizungumza Mheshimiwa Monica Mbega alisema *SACCOS* kwa kawaida zinawalenga watu wa kati na haziwafikii watu wa chini kwa hiyo, vikoba inaweza kuwa ni suluhihisho na kuhakikisha kwamba tunawafikia wale watu wa chini ambaa ndiyo wengi zaidi na ndiyo ambaa walikuwa wamekusudiwa katika fedha za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, hoja ya thelathini na nne, Shirika la Hifadhi la Jamii *NSSF*. Serikali iharakishe utekelezaji wa mradi wa daraja la Kigamboni na uanze kabla ya mwaka 2010 na usimamizi wake uwe chini ya *NSSF*. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifani, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, Mheshimiwa Mzee Ngwali Zubeir. Mchakato wa uendeshaji wa mradi wa Daraja la Kigamboni, umeanza kwa tangazo la kutafuta mbia lilitolewa tarehe 17 Julai, 2008. Ushauri wa kuweka ratiba kamili wa utekelezaji wa daraja la Kigamboni utazingatiwa na tutaitangaza. Utambuzi wa changamoto za utekelezaji wa mradi utafanywa mapema na kuwekewa mikakati. Kwa kupitia Wizara ya Ardhi, Maendeleo ya Makazi, tayari Serikali imeanza kulipa fidia kwa wakazi wa maeneo ya mradi wa Daraja la Kigamboni mpaka sasa wamekwishalipa shilingi bilioni 250.

Mheshimiwa Spika, hoja ya thelathini na tano, waajiri wasioandikisha watumishi wao kwenye Mifuko ya pensheni wachukuliwe hatua za kisheria. Hii imetolewa na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Wizara kwa kupitia Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii itahakikisha kuwa hatua zinazopaswa zinachukuliwa dhidi ya waajiri wanaobainika kukiuka taratibu hizi. Hatua hizo ni pamoja na kuwapeleka Mahakamani kwa mfano mwaka 2007/2008 waajiri 85 walifikishwa Mahakamani kwa sababu hiyo. Mwenendo wa kesi hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kesi 60 *NSSF* imeshinda Mahakamani, kesi 15 makubaliano yamesainiwa nje ya Mahakama ambako waajiri wanalipa michango kidogo kidogo na kesi 10 bado zinaendelea Mahakamani. *NSSF* itaendelea kushirikiana na Idara ya Kazi na Vyama vya Wafanyakazi kuhakikisha kuwa waajiri wanawaandikisha wafanyakazi wao katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Hoja nyingine inayofuata *NSSF* iharakishe ujenzi wa Ofisi ya Ubalozi Nairobi nchini Kenya na nchi nyingine. Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifani ambaye ndiye alikuwa Msemaji Mkuu wa Upinzani, napenda kumjibu kwamba tangazo la kupata wataalamu washauri kwa ajili ya ujenzi wa Ubalozi wa Tanzania nchini Kenya lilitolewa tarehe 21 Aprili, 2008, maombi ya wataalamu washauri yalifanyiwa uchambuzi na kuonekana kuwa wengi walishindwa kukidhi masharti ya zabuni kufuatana na Sheria ya Manunuzi. Kutokana na sababu hizo, zoezi hili litarudiwa mwishoni mwa mwezi huu.

Pia kulikuwa na hoja kwamba *NSSF* iharakishe utekelezaji wa mradi wa Chuo Kikuu cha Dodoma ambayo ilitolewa na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalifani, Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa hosteli kwa wanafunzi 5,000 iko katika hatua za mwisho na ujenzi utakamilika mwezi Septemba, 2008. Awamu ya pili, ya ujenzi wa madarasa, majengo ya miadhara, semina, mabwalo ya chakula na zahanati utaanza mwezi huu na kumaliza kabla ya mwisho wa mwaka huu.

Pongezi na shukrani kwa *NSSF* kwa ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na ujenzi wa jengo la Wamachinga Dar es Salaam, nyumba za Jeshi la Wananchi, nyumba za Polisi, nyumba za bei nafuu na miradi mingine kama hiyo. Kulikuwa na ushauri kwamba Majengo kama hayo yajengwe katika Mikoa mingine. Hoja hii imetolewa na

Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Janeth Massaburi, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Christant Mzindakaya, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Abass Mtemvu, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegriy, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Maria Hewa na Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni.

Mheshimiwa Spika, pongezi za utekelezaji wa miradi hii tunazipokea na *NSSF* wapo wanazisikia, Wizara itaendelea kuisimamia *NSSF* ili iendelee na kazi nzuri wanayoifanya, juhudzi zinafanyika kujenga majengo mengine kama haya katika Mikoa mingine kwa kushirikiana na Halmashauri za Miji, Wilaya kwa misingi ya kibashara.

Mheshimiwa Spika, jengo la Machinga litunzwe vizuri, Mheshimiwa Bujiku Sakila ndiyo hoja yake. Bodi imeundwa kusimamia uendeshaji wa jengo hilo. Bodi hii inawahusisha wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Wamachinga wenywewe na *NSSF*.

Hoja iliyofuata ni *NSSF* ishirikiane na Halmashauri za Wilaya au Miji kujenga nyumba za bei nafuu na majengo ya wafanyabiashara. Wafanyabiashara na wazalishaji wadogo wadogo kuondoa kero za makazi na kuleta maendeleo. Kwa mfano Kwimba, Ukerewe, Kibondo, Sumbawanga, Misungwi, Mwanza, Dar es Salaam bila ya kusahau hoja ya Mheshimiwa Spika na Urambo.

Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Janeth Massaburi na Mheshimiwa Samwel John Sitta. *NSSF* itafanya mawasiliano na uongozi wa Mawilaya, Miji kuangalia namna ya kutekeleza miradi hiyo katika misingi ya kibashara. Hoja iliyofuata ni *NSSF* iangalie uwezekano wa kusaidia *Faraja Women Group* ya Dodoma kuendeleza kiwanja chao. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Balozi Getrude Ibengwe Mongella. *NSSF* itafanya mawasiliano na kikundi kinachohusika kuona iwapo mradi huo unatimiza au unaendana na vigezo vyta uwekezaji wa *NSSF*.

Hoja namba 60 ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana ishughulikie matatizo ya madai ya muda mrefu ya wafanyakazi wa Makampuni ya *Mbeya Industries* tokea mwaka 1998, Zana za Kilimo kwa miaka saba sasa na *Mbeya Cement Company Limited*, hii ilikuwa inahusu mafao. Kufuatana na kumbukumbu zilizopo katika ofisi za *NSSF* Mbeya hakuna madai yoyote yenye matatizo yanayohusiana na wafanyakazi wa Makampuni yaliyotajwa. Inawezekana kuwa wafanyakazi wenye malalamiko haya ni wa mifuko mingine. Wizara itawasiliana na mifuko mingine ya pensheni kufanya uchunguzi na kuchukua hatua zinazostahili.

Hoja nyingine ni miradi ya *NSSF* inawanufaisha vipi wanachama wake? Hili limeelezwa na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda. Wanachama wanafaidika kwa kupitia mafao wanayoyapata ambayo ni ya muda mfupi na ya muda mrefu. Pia Shirika linawekeza katika miradi mbalimbali ambayo inawapatia ajira wananchi ambaa wengi wao ni wanachama. Vile vile Shirika limejenga nyumba za bei nafuu eneo la Kinyerezi

Dar es Salaam ambapo wanachama walipewa kipaumbele katika kuzinunua, mradi kama huu utatekelezwa eneo la Kigamboni mwaka huu kwa makusudi hayo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ihmize kujenga nyumba za bei nafuu na hatimaye barabara kwa mkataba na Serikali. Yaani anachoshauri Mheshimiwa Mbunge hapa vile vile si tu *NSSF* iishie katika kujenga nyumba za bei nafuu, lakini vile vile waanze kujenga barabara kwa kuingia mikataba na Serikali. Hii imetolewa na Mheshimiwa Pindi Chana. Kama nilivyoeleza hapo juu Mashirika *NSSF* na *PPF* tayari yanawekeza katika ujenzi wa nyumba hasa nyumba za gharama nafuu. Tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kuyataka sasa kuingia hata katika ujenzi wa barabara kwa mkataba na Serikali. *NSSF* wameanza na daraja la Kigamboni pengine huo ni mwanzo mzuri. Ushauri huu tutaufanyia kazi na tutaangalia Serikali wanatuelekeza vipi.

Kulikuwa kuna hoja ya Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya kwamba *NSSF* ingekuwa vizuri vile vile wakaanza kushirikiana na wawekezaji binafsi hasa wale ambao hawana uwezo lakini wanakuwa na mitaji yao kama vile ardhi au nyumba. Suala hili tutalifikisha katika Bodi ya *NSSF* na kuangalia jinsi ambavyo linaweza likashughulikiwa kibashara. Shirika la Tija (*NIP*), hoja iliyokuwepo ni kwamba suala la Kiwanja cha *NIP* Mbezi, Kiwanja Na. 906/H. Hoja imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Haroub S. Masoud.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia ya kiwanja namba Sh. 11,370,000/= zilizobakia kutokana na msukumo wa Wizara yangu na Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeiandikia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili iwasiliane na *IMTU* kuhusiana na fidia iliyobakia. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu nayo tayari imeshawaandikia *IMTU* na kuagiza kulipa fidia iliyobakia kwa *NIP* na kuwaambia wazi kwamba msipolipa itabidi wanyang'anywe kiwanja. Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana inaendelea kufuatilia suala hili.

Kuhusu kuiondolea *IMTU* milki ya kiwanja hicho kwa kutokiendeleza kwa zaidi ya miaka mitatu, Wizara yangu itawasilisha suala hili na kufuatilia kwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi sanjari na suala la uwezekano wa kiwanja hicho kurudishwa *NIP*. Kwa sababu wakati *NIP* inanyang'anywa ilikuwa angalau ilishajenga nyumba angalau ilikuwa haijakamilika lakini imeshajengwa nyumba na ilikuwa imeshajengwa uzio hawa hawajafanya chochote tangu wamepewa. Kwa hiyo, ni dhahiri kama watu wanasema sheria ni msumeno lazima ikate mbele na nyuma.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Tija, Mheshimiwa Jenista Mhagama ndio ilikuwa hoja yake, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Tija la Taifa imeanza mchakato wa kutengeneza Sera ya Taifa ya Tija, mchakato huo umetegemewa kuchukua miaka mitatu hadi kukamilisha kutokana na kuhusisha wadau mbalimbali wa nje ya nchi. Kuwezesha Wakala wa Usalama na afya mahali pa kazi ili uweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kwa ufanisi, kwa sababu hoja ilikuwa kwamba *OSHA* haina meno wala nguvu. Hoja ile ilitolewa na Mheshimiwa Abdallah Khalfani na Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame. Katika kuiwezesha *OSHA* ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi Serikali

imeanzisha mchakato wa kutunga Sera ya Taifa ya Usalama na Afya mahali pa kazi, Sera hiyo itaipa *OSHA* nguvu zaidi ya kutekeleza majukumu yake pia katika sera hiyo kuna tamko maalum la kuanzisha Mfuko wa Kuzuia Ajali na Magonjwa sehemu za kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali vile vile kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inaendelea na mchakato wa kurekebisha Sheria za Usalama na Afya mahali pa kazi ili kuipa *OSHA* nguvu zaidi kutekeleza majukumu yake. Ili kuweza kuyafikia maeneo mengi zaidi ya nchi *OSHA* imeanzisha kanda sita ambayo Makao Makuu yake yatakuwa ni Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Dar es Salaam na Mtwara. Ili kuongeza kasi ya utendaji kazi Serikali imeanza kuajiri Wakaguzi zaidi ili kutekeleza majukumu hayo. Pia Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kutoa vitendea kazi mfano usafiri, mawasiliano na vifaa vya kitaalamu ili kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, sasa naingia Idara ya Maendeleo ya Vijana, hoja iliyojitokeza ya kwanza ilikuwa hatua iliyofikiwa kuhusu utoaji wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana. Tuna Mfuko na tuna zile fedha za Mheshimiwa Rais na tuna fedha za Mfuko wa Vijana ambaa huu ulikuwa unatolewa tangu siku nyingi. Mheshimiwa Mgana Msindai anauliza kuhusu hatua iliyofikiwa katika utoaji wa mikopo kwa vijana iliyokuwa inatolewa na Wizara yangu kupitia Halmashauri za Wilaya bado inaendelea kutolewa kilichobadilika ni utaratibu tu wa utoaji mikopo hiyo. Kwa sasa mikopo hiyo inatolewa kupitia *SACCOS* kila Wilaya imeagiza kuleta majina *SACCOS* mbili zitakazotoa mikopo kwa vijana katika Wilaya. Orodha ya majina ya Wilaya zilizowasilisha majina ya *SACCOS* zimeonyeshwa kwenye jedwali Na. 7 lililoambatanishwa kwenye hotuba yangu.

Ni vijana wachache sana wenye ulemavu waliofaidika na Mfuko huu wa Vijana. Swali hili limeulizwa na Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga. Kuhusu hoja kuwa watu wenye ulemavu wachache kufaidika na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana tunakubaliana na hoja hii. Tutaendelea kuhamasisha vijana wenye ulemavu ili wajitokeze kupata mafunzo ya ujasiriamali na wajunge kwenye Vyama vya Ushirika, Akiba na Kukopa *SACCOS* ili iwe rahisi kwao kupata mikopo ya vijana chini ya utaratibu wa sasa ambaa fedha hizi zitatolewa kupitia *SACCOS*. Tunachoomba ni kwamba Halmashauri nazo ziwatambue kwamba vijana wenye ulemavu ni kipaumbele wasiwaone kwamba wao ni watu ambaa kazi yao ni kuombaomba. Wanao uwezo kabisa wa kufanya kazi na kuzalisha kama binadamu wengine wote wakiwezeshwa. (*Makofî*)

Hoja nyingine iliyotolewa ni kwamba Wizara kusaidia vikundi vya vijana Wilaya ya Ludewa. Hii ilitolewa na Mheshimiwa Mwalyosi. Wizara inawapongeza vijana Ludewa kwa kuunda vikundi vya kuzalisha mali katika shughuli za kutengeneza boti na vyungu. Wizara yangu inashauri vijana hawa wawasiliane na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ili shughuli zao ziweze kutambulika na kuwa endelevu. Aidha, wawasiliane na Halmashauri ya Wilaya ili iweze kushiriki katika maonesho mbalimbali kama maonesho ya Saba Saba, Nane Nane na Wiki ya Vijana kama njia ya kutangaza shughuli zao na kupanua wigo wa soko. Kama hivi leo hapa tuna maonesho vijana hao wangekuwepo hapa wangeweza kufaidika vile vile na pengine wangeweza hata kupata wazo la kwenda Kigali Rwanda.

Marejesho hafifu ya fedha za vijana, hili limeulizwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah. Hii ni kweli lakini Wizara inafuatilia na itaendelea kufuatilia marejesho hayo kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya. Aidha, Wizara inakubaliana na ushauri kuwa fedha zinazotolewa kwa baadhi ya vikundi ni ndogo. Hata hivyo, kwa sasa cha msingi ni waliokopa kurejesha fedha hizo. Wizara imelenga kuboresha matumizi ya fedha za Mfuko huu kwa kubadilisha utaratibu wa utoaji wa mikopo hiyo kupitia *SACCOS*. Hata hivyo, Wizara inashauri Halmashauri zitoe fedha za mikopo kulingana na mahitaji ya miradi.

Hoja nyingine iliyojitokeza ni uundwaji wa Baraza la Vijana la Taifa. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Said Amour Arfi. Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na Baraza la Taifa la Vijana na tayari imeanza mchakato wa kuunda Baraza hili kwa kuwashirikisha vijana wenyewe kutoka vikundi na Taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali pamoja na wadau wengine wa vijana katika maandalizi ya mkakati wa kuunda Baraza hili. Aidha, kufuatia mapendekezo ya Mikutano miwili ya wadau imeonekana kuwepo na umuhimu wa kushirikisha vijana zaidi hasa kutoka maeneo ya vijijini ili kufanya uundaji wa Baraza kupata ushiriki wa vijana Kitaifa kabla ya kuandaa Sheria ya uundaji wa Baraza hili. Aidha, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Jenista Mhagama wa kuharakisha mchakato wa kisheria wa kuunda Baraza hili kwenye Kamati yake.

Hoja nyingine kuna tatizo kubwa la utumiaji wa dawa za kulevyta ni hoja ya Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo na Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis. Serikali inatambua kuwa kuna wimbi kubwa la vijana ambao wamejihusisha na utumiaji wa dawa za kulevyta kwa kutambua hivyo Serikali ilianzisha Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevyta chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tume hii inashirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali katika suala zima la kuzuia kilimo, uzalishaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevyta. Aidha, Wizara inashirikiana na Tume katika kutoa elimu ya kupambana na matumizi ya dawa za kulevyta hasa kwa vijana. Tume pia ina mpango wa kujenga kituo kwa ajili ya waathirika wa dawa za kulevyta hapa Dodoma. Lengo kubwa ni kuzuia matumizi ya dawa hizi.

Tafsiri ya kijana hili liliulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar anasema inaleta mkanganyo kwa sababu wako watu hata wa miaka 50 wanajiita vijana. Mimi nadhani wa miaka 50 watu wanasema *life begins at fifty*, sasa nadhani inakubalika. Lakini kuna tafsiri mbalimbali kuhusu kijana, hakuna tafsiri inayofanana duniani, tafsiri ya kijana inategemea mtazamo wa nchi, sera au sheria na hata mila na taratibu. Umoja wa Mataifa unatambua kijana kama mtu mwenye umri kati ya miaka 15 hadi 24. Hapa nchini Tanzania Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana inaanisha umri wa kijana kuwa kati ya 15 hadi 35. Hivyo Mpango wa Maendeleo ya Vijana inahusu vijana walio katika umri wao, kwa hiyo, inategemea hata miaka 40 au 50 kumbuka maneno ya Mzee Kenyatta. (*Makofi*)

Hoja nyingine umri wa Serikali kushirikiana na *SIDO* kuwajengea uwezo wa kuijajiri vijana kwa kuwapatia elimu na ujuzi wa kutengeneza vifaa vidogo hili liliulizwa na Mheshimiwa Aziza Slyem Ali. Wizara inatambua na kuthamini sana

mchango wa *SIDO* katika kuwajengea vijana uwezo wa kujajiri kwa njia ya mafunzo ya ujuzi wa aina mbalimbali. Kwa kuzingatia suala hili Wizara kwa muda mrefu imekuwa na ushirikiano wa karibu sana na *SIDO*.

Elimu ya UKIMWI bado haitoshi hilo liliulizwa na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda. Nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi mjini na vijijini bila ubaguzi na kuhamasisha wazazi kutoona aibu kuongea na watoto wao juu ya masuala ya UKIMWI. Aidha, Wizara inaelimisha na itaendelea kutoa elimu ya UKIMWI mahali pa kazi pamoja na kutoa misaada na huduma kwa watumishi walioathirika. Vile vile hoja hii ilikuwa imechangiwa na Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Dr. Lucas Siyame.

Umuhimu wa mafunzo kwa vijana hilo liliulizwa na Mheshimiwa Janet Massaburi, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah na Mheshimiwa Thomas Mwang'onda. Nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kuwa ili vijana waweze kujajiri wanatakiwa kupata elimu ya kujitegemea, elimu ya ufundi na stadi nyingine. Wizara hutoa mafunzo haya kwa kushirikiana na Taasisi za Mafunzo kama vile *SIDO*, VETA na nyinginezo ili kuboresha uzalishaji katika shughuli za vijana na biashara za kilimo na ufundi. Aidha, Serikali hutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana.

Shughuli za Maendeleo ya Vijana kuendeshwa na vijana wenyewe hilo liliulizwa na Mheshimiwa Juma Killimbah. Suala la Maendeleo ya Vijana ni suala mtambuka linahitaji ushirikiano wa sekta mbalimbali na watu wetu wenye taaluma mbalimbali. Kwa misingi hiyo hata watendaji waliopita umri wa vijana wanaweza kuwaongoza vijana la msingi ni kujenga utaratibu wa ushirikiano baina ya Taasisi na sekta mbalimbali.

Hoja namba 44 matumizi ya Kituo cha Vijana Sasanda Mbozi Mbeya ameuliza Mheshimiwa Godfrey Zambi - Mbunge wa Mbozi Mashariki. Mheshimiwa Zambi atakumbuka hoja hii aliitoa mwaka jana pia na Wizara ikamweleza kuwa kituo cha Sasanda kimetengwa maalum kwa ajili ya maendeleo ya vijana. Wizara inatambua umuhimu wa kuwaendeleza vijana waliohitimu elimu ya msingi na sekondari wapate ujuzi wa kushiriki katika shughuli za uzalishaji. Lakini tunaendelea kukuomba na kusisitiza kuwa shughuli za vijana zinazoendelea hapo ni muhimu sana pia.

Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara ilitenga Sh. 50,000,000/= ambazo zimefanya kazi zifuatazo:- Imefanya ukarabati wa daraja, imeendesha mafunzo ya wajasiriamali na kuajiri watumishi wawili kwa ajili ya kituo hicho. Aidha, kituo kimeshafanya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendesha Makambi ya Kazi ya Vijana, Wizara inahitaji kituo hiki kwa ajili ya mafunzo ya nadharia na vitendo kwa vijana katika nyanja za kilimo, ufugaji na utunzaji mazingira. Katika mwaka huu wa fedha Wizara imetenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa majengo na kuimarisha miundombinu. Mahitaji halisi yataainishwa wakati wa kuanza taratibu za ujenzi.

Uanzishwaji wa dawati la shughuli za vijana katika ngazi za vijana katika ngazi ya Wilaya, hili liliulizwa na Mheshimiwa Monica Mbega na Mheshimiwa Mgana Msindai. Ni kweli tuna tatizo la kupata uwakilishi katika ngazi ya Wilaya. Lakini tunashukuru kwamba kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI sasa suala hilo tumeanza kulitatua na ziko Halmashauri ambazo tayari zimeshatangaza kutoa nafasi kwa maafisa vijana. Halmashauri ya Mufindi, Manispaa ya Ilala, Lindi Vijijini, Arusha, Bagamoyo, Pangani, Singida na Wizara itaendelea kuhamasisha Manispaa nyingine kufanya hivyo.

Kuhusu vijiwe, hilo tunaendelea nalo ilikuwa ni hoja ya Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya. Mpaka sasa baadhi ya vijiwe vimeanza kutumika hata katika shughuli za kupambana na UKIMWI na Polisi Jamii. Kuwe na mpango mkakati wa maendeleo ya vijana limezungumzwa na Mheshimiwa Mzindakaya na Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfani. Nimeshazungumza wakati nilipokuwa nafafanua kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama *ILO* na *UNDP*. Umuhimu wa vijana kutengeneza maeneo ya kufanyia kazi ni kweli ni tatizo hasa kama miji kama Dar es Salaam vijana wanapigwa utadhani kondoo au mbuzi, lakini ni kweli kwamba vijana wengi waliopo maeneo ya mijini wanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maeneo ya kazi. Wizara itaendelea kuwasiliana na Halmashauri za Miji ili waweze kuwatengea maeneo na hasa baada ya kujenga miundombinu. Kutoa huduma kwa vijana mijini hili tumeshalijibu. Kuongezeka kwa mmonyoko wa maadili kwa vijana na masuala ya utandawazi. Hii ni kweli inabidi sasa wazazi tukae macho tunapowaruhusu watoto wetu kuangalia televisheni.

Mheshimiwa Spika, ulipokuwa haupo nilipokuwa naanza kutoa hoja yangu nilikushukuru sana wewe kwa jinsi unavyoendesha shughuli za Bunge hili kwa maana ya *standard and speed*. Narudia tena kutoa pongozi hizo na baada ya wewe kutoa kauli hiyo ya *standard and speed* mambo mengi utayaona katika nchi hii sasa yanakwenda kwa *standard and speed*. Kwa mfano hata ukizingatia mechi ya jana kati ya Simba na Vitallo ile *speed* ilikuwa sio ya kawaida. Kwa hiyo, tunachukua nafasi hii kuwapongeza sana vijana wetu wa Simba kwa kuonyesha mpira mzuri jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, napokea kwa unyenyekevu mkubwa pongozi zako juu ya tunavyoendesha kazi.

Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyio mbele yetu ni ya kuitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana. Kile kibwagizo kuhusu Simba hakihusiki na hoja hii kwa sasa. Ingawa kama mnavyofahamu, Spika anafurahia sana vijana wale wanapofanya vizuri.

Sasa hoja hii ili iamuliwe tunapitia katika utaratibu ambao Katibu atatutangazia.

## **KAMATI YA MATUMIZI**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

#### **Fungu 15 – Tume ya Usuluhihi na Uamuzi**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... Shs. 1,445,351,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati Ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 65 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana**

Kif. 1001 – *Administration and General* ... Shs. 1,761,473,500/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Said Amour Arfi na Mheshimiwa Susan Lyimo. Tutaanza na Mheshimiwa ...ah, eeh ndio na Mheshimiwa Manyinyi, basi labda tuanzie kulia. Mheshimiwa Manyinyi.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kifungu hicho *vote 65*, programu 10 *sub-vote 1101 – 250100 – Mshahara wa Waziri*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kukubali kuja jimboni kwangu Musoma kwa ajili ya kumaliza ile migogoro iliyopo kati ya watumishi na wenyewe viwanda vile vya Samaki lakini hali kadhalika na Kiwanda cha Nguo cha *MUTEX*.

Pamoja na kukubali kwake, ningependa kufahamu kama Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari tuweze kuongozana pindi Bunge tu litakapomalizika kabla hajaongozana na Mheshimiwa Aziza.

**MWENYEKITI:** Unampangia ratiba! haya. Basi Waziri sijui unasemaje kuhusu hilo?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kukubali mwaliko wa Mheshimiwa Manyinyi, naahidi kwamba tutafuatana naye, lakini siwezi kuwa *very definite* yaani kwa uhakika tukimaliza Bunge hili tuendelee kusafiri kwa sababu itategemea na ratiba nyingine za Serikali vile vile. Kwa hiyo, nitaanza naye kabla ya Mheshimiwa Aziza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu kuhusu hotuba hii pamoja na kwamba hoja nyingi Mheshimiwa Waziri amejitahidi kuzitolea maelezo nampongeza sana, lakini napenda nipate ufanuzi katika maeneo mawili.

La kwanza katika mchango wangu nilizungumzia kuhusu wimbi kubwa la vijana ambao wamejihusisha na madawa ya kulevya. Kwa kweli wamekuwa ni kero kwa nchi hii wenye familia na jamii kwa ujumla. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ina mpango gani kuandaa kituo kwa ajili ya kukusanya hawa vijana ambao sasa hivi wanasumbua sana kwenye familia mbalimbali? Nilikuwa nahitaji nipate ufanuzi kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilikuwa nimemwomba Mheshimiwa Waziri kwamba baada ya kuona kazi nzuri inayofanywa na NSSF kwa kujenga majengo mbalimbali maeneo mbalimbali kama yale tuliyoyaona Chuo Kikuu, niliwasiliana na Mkuu wangu wa Mkoa akaniomba nichangie kwamba ni lini sasa Waziri ataelekeza nguvu hizo Singida kwa sababu Singida tuna ardhi nzuri, tena pana, haina gharama na tuna uhaba wa nyumba za kukaa na vile vile tuna uhaba wa ofisi mbalimbali. Nilikuwa nimeomba kwamba Mheshimiwa Waziri aseme Singida lini mradi huo atauleta? Ahsante. (*Makofii*)

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Chilolo kama ifuatavyo:-

Kuhusu madawa ya kulevya nilieleza katika hoja na nimejibu katika ufanuzi hapa kwamba sisi Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana tunashirikiana na Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya. Tume hiyo katika utaratibu wake imeshajipangia kujenga kituo hapa Dodoma ili kuwakusanya vijana hao na kuweza kuwapa ukarabati au *rehabilitation* ili waweze kupata unafuu. Kwa hiyo, mipango ipo na imekwishaanza na Tume ile ina bajeti yake inajitegemea, lakini tunashirikiana nao kwa sababu sisi ndio wenye sera.

Mheshimiwa Spika, kuhusu NSSF lini inakwenda Singida? Nilipokuwa nikijibu vile vile nimesema NSSF iko tayari kushirikiana na Halmashauri za Miji au Manispaa au Majiji, wanachohitaji ni kupata mwaliko rasmi, halafu watakuja kufuatana na mialiko ile, mtakaa nao mtafanya tathmini. Kwa hiyo, ratiba ni lini, itategemea mwaliko unafika lini.

**MWENYEKITI:** Kuhusu kuandaa miradi, maana yake kama hamna miradi mnasema tu mna ardhi nzuri inaweza kuwa shida.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Awali ya yote napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, karibu amejibu hoja zangu zote katika mchango wangu wa maandishi, lakini eneo moja nilikuwa nahitaji nipate ufanuzi.

Nilizungumza kuhusu hawa wawekezaji na mishahara ambayo wanatoa kwa wafanyakazi wa Kitanzania. Lakini pia nilizungumzia kuhusu wafanyakazi wanaofanya kazi katika Makampuni ya Tumbaku ya ATTT wanapata mishahara midogo sana baada ya kutoa makato wanabakiwa kama na Sh. 58,000/= hivi. Lakini kibaya zaidi, wafanyakazi hawa wanafanya kazi katika maghala ya tumbaku ambayo wanahatarisha afya zao, hawana mavazi na wala hawapimwi afya zao. Wizara ina maelezo gani kuhusu eneo hili la wafanyakazi wanaofanya kazi katika mazingira yanayohusu Tumbaku?

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni kweli kwamba mishahara wanaolipwa wafanyakazi walio katika Shirika la ATTT ipo chini ya kima cha chini kilichotangazwa na Serikali. Naomba niseme kwamba tukimaliza Bunge, tutapeleka Wakaguzi pale ili kuthibitisha hali hiyo na baada ya hapo hatua za kisheria zitachukuliwa.

Lakini la pili, kuhusu mazingira, *OSHA* wamesikia, naipokea taarifa hii na tutaifanya kazi, kwa sababu tumeshapata matukio mbalimbali katika sehemu mbalimbali za nchi ambapo wafanyakazi wameweza hata kupoteza fahamu kutokana na madawa ambayo wanayatumia pale. Sasa tumbaku inawezekana isiwe ni ile dawa ambayo inamfanya mtu apoteze fahamu, lakini ukiwa unapata ule mvuke wake kila mara athari yake vilevile itajitokeza huko mbele ya safari. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba *OSHA* wanawakagua wafanyakazi wale na kuhakikisha kwamba wanawaelekeza na kuchukua hatua zinazodhibiti. Kama itabidi kufunga shughuli zao kwa muda watafungiwa kwa muda.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweza kujibu hoja zetu kwa ufasaha. Lakini nilikuwa naomba anipe ufanuzi katika masuala mawili ambayo katika mchango wangu nilikuwa nimeuliza. Ni kweli kwamba kigezo cha kutambua kundi la watu ni gumu na mimi ninavyoju, Sera ya Maendeleo ya Vijana inamtambua kijana kuwa na umri kati ya miaka 15 mpaka 24 na sera hiyo ninayo hapa. Lakini Mheshimiwa Waziri amesema kwamba anamtambua kijana kutoka miaka 15 mpaka miaka 35. Sasa naomba maelezo, ni kwanini kuna hizi tofauti au Mheshimiwa Waziri alikuwa ana maanisha sera za vijana wa CCM kwa sababu vijana wa CCM ni miaka ndiyo miaka 15 mpaka 35?

Suala la pili, ninaomba kupata ufanuzi kuhusu suala zima la wimbi wa vijana kutoka vijijini kwenda mjini ambalo ni tatizo kubwa linalopelekea vijana hao kuja mjini ni suala zima la kutokuwa na miundombinu mizuri katika vijiji ikiwemo masoko, sehemu za burudani na vinginevyo.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri atuambie Wizara yake inamikakati gani ya kuhakikisha kwamba inawekeza vijijini ili kupunguza wimbi hili la vijana kwa sababu kwa kweli wanapokuja mijini wanaleta matatizo makubwa ikiwepo na kutokuwepo na maadili, lakini pia kuingia kwenye vitendo vingine vibaya kama kuvuta bangi, uhuni na mengineyo.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umri wa vijana, nilipokuwa nafafanua hapa, nilikiri kwamba ziko tafsiri mbalimbali za vijana. Ipo tafsiri ya miaka 15 mpaka 24, iko tafsiri ya 15 mpaka 35. Nikasema inategemea na mtazamo au Sera. Sera ya Serikali anayoizungumzia Mheshimiwa Susan Lyimo yenye kumtambua kijana kuwa ni mwenye umri wa miaka 15 hadi 24. Sera mpya ya sasa hivi inazungumzia kijana kuwa na umri kati ya miaka 15 mpaka 35.

Unajua Sera hizi zinaendana na mazingira. Wakati tulipopata uhuru ilikuwa ukimwangalia mtu mwenye miaka 30 anaonekana ni mtu mzima kweli kweli. Sasa hivi ukimwangalia mtu mwenye miaka 30 haki ya Mungu unaweza ukasema ni mtoto. Sasa ndiyo tunavyokwenda. Ndiyo maana tunasema inaweza ikafika wakati hata yule wa miaka 50 akaonekana ni kijana kutokana na mazingira. Ndiyo maana methali za Wazungu zinasema: “*Life begins at forty or life begins at fifty*” kwa sababu unapofika miaka 50 ndiyo kwanza unaonekana unaanza kuchanua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuna lile la pili alilouliza bado hujajibu.

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ajira na suala la vijana ni suala mtambuka. Ni suala ambalo Serikali nzima inahusika. Kwa hiyo, tunapozungumza kuwekeza miundombinu, tunazungumzia Waziri wa Miundombinu, rafiki yangu yupo hapa anasikia, tunapozungumza suala la kujenga nishati. Waziri wa Nishati amejibu maswali hapa leo, anasikia ili kuhakikisha kwamba ile Sera yetu ya umeme vijijini unakwenda na Wizara nyingi zinahusika. Lakini vilevile tunaomba wawekezaji binafsi nao wajielekeze huko.

Sasa hivi tumeanza kupata mwamko kwamba unakuta wawekezaji binafsi hasa kutoka kwenye makampuni ya nje kwa mfano kwa wale wanaotaka kulima *bio fuel* kule Mkuranga. Mimi nina hakika kama kile kiwanda kikifanikiwa kule Mkuranga utakuta vijana wengi wa Mkuranga badala ya kuja Dar es Salaam au Kibaha watabaki kule kule Mkurunga. Kwa hiyo, ni suala ambalo Serikali nzima tunalishughulikia na tunalitazama kwa uangalifu sana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* . . . . . shs 189,623,800/=

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* . . . . . shs 365,108,100/=

Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit* . . . . . shs 111,827,500/=

Kifungu 1005 - *Procurement Managemetn Unit*.. shs 188,475,900/=

Kifungu 1006 - *Inf, Education and Comm. Unit* ...shs 85,118,200/=

Kifungu 2001 - *Labour* . . . . . shs 1,789,524,500/=

Mheshimiwa Spika, uwezo wa NSSF unajionyesha dhahiri katika ushiriki wake katika ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. Uwezo huu unatisha na ninawapongeza kwa dhati.

Kifungu 2002 - *Employment Division* . . . . . shs 857,414,500/=

Kifungu 2003 - *Registrar of Trade Unions* . . . . . shs 165,416,100/=

Kifungu 5001 - *Youth Development* . . . . . shs 1,000,623,900/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

## **MIPANGO YA MAENDELEO**

## Fungu 65 – Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... shs 378,845,000/=  
Kifungu 1003 - *Policy and Planning*.... .... .... shs 2,375,000,000/=  
Kifungu 2001- *Labour* .... .... .... .... .... shs 1,444,861,500/=  
Kifungu 2002 - *Employment Division* .... .... .... shs 1,533,612,000/=  
Kifungu 5001 - *Youth Development*... .... .... .... shs 480,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

(*Bunge lilirudia*)

TAARIFA

**WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa Wizara ya kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2008/2009 na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Iilitolewa Iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka 2008/2009 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huwa inarahisisha sana kuyapitisha ikiwa Waziri anakuwa makini katika kujibu kama alivyoonyesha Waziri huyu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kuna matangazo mawili tu. Tangazo la kwanza ni kwamba kesho tutakuwa na mgeni ambaye ni Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa - Dr. Asha Rose Migiro na Kamati ya Uongozu na Tume ya Huduma ya Bunge inakwenda kukutana hivi sasa ili kuandaa utaratibu ambao kesho asubuhi tutawaelezeni utaratibu huo utakuwaje jinsi ya kumpokea na aweze kuzungumza nasi.

Tangazo lingine ni kama nilivyo sema kwamba, hotuba ya mto hoja - Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika ni kesho. Kwa hiyo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi kesho.

*(Saa. 05.45 Asubuhi Bunge lilahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne,  
Tarehe 22 Julai, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*